

CONSTITUTION OF KENYA REVIEW COMMISSION

(CKRC)

Verbatim Report Of

**DISSEMINATION OF REPORT AND DRAFT BILL, MWALA
CONSTITUENCY, HELD AT MAKUTANO AIC CHURCH**

ON

7TH OCTOBER, 2002

**DISSEMINATION OF REPORT AND DRAFT BILL, EASTERN PROVINCE – MWALA CONSTITUENCY,
AT MAKUTANO AIC CHURCH ON 7TH OCTOBER, 2002**

Present:

Mrs. Abida Ali Aroni - Commissioner

Secretariat Staff in attendance:

Collins Mukewa - Programme Officer
Susan Mutile - Verbatim Recorder

The meeting started at 11.40 am with a prayer led by Rose Kikonyo. The District Coordinator, Rose Kimeu, introduced committee members.

District Coordinator: (*In Kikamba*)

Rose Kikonyo: (*Prayer in Kikamba*)

District Coordinator: Na basi kwa wakati huu ningetaka kuanza mkutano wetu wa leo na kwanza kabisa ningependa

kuwajulisha wageni wetu ambao wamefika hapa kutoka Nairobi, na tutaanza na Commissioner mwenye amefika hapa leo, atajitambulisha kwenu halafu atawatambulisha wale watu wengine amekuja nao na tutaendelea.

Com. Abida Ali Aroni: Hamjambo? Kwa niaba ya Tume ya Marekebisho ya Katiba, ningependa kuwalika kama mumevyoalikwa na the Coordinator, mimi naitwa Abida Ali Aroni, ambaye ni naibu wa Mwenye Kiti na nimeandamana na Programme Officer, Collins Mukewa, ambaye tutasaidiana kwa hii kazi, na mtu atakayekuwa ana nasa sauti zetu na ku-record ni Susan Mutile. Asanteni.

District Coordinator: Na mimi ni matumaini yetu kwamba wengi wetu mnanijua, mimi naitwa Rose Ngina Kimeu, District Coordinator wa Review Commission Machakos. Na kati yetu pia tuna wale members wa Constituency Committee ya hapa Mwala. Wenyenye mmefika mkaweze kusimama tuwatambulishie. Constituency Committee Members wale mko nao hapa pengine mtaanza kujitambulisha kutoka pale na wale wengine.

Cllr. Musau: (*In Kikamba*) Kwa jina naitwa Cllr. Ngaratu Musau, Masaku County Council.

Juliana: Kwa jina naitwa Juliana Teresia Muli, mimi ndiye nasimamia vikundi vya akina mama.

Anastasia: Kwa jina naitwa Anastasia Ngonzi kutoka upande wa Mbiuni.

Cllr. Musau: Ile ingine nilikuwa nataka kuwajulisha katika District hii ya Machakos, mimi ndiye nilichaguliwa kuenda katika National Constitutional Conference. Asante.

District Coordinator: Sasa ni wakati wetu tupatia Commissioner Abida Ali Aroni wakati aweze kuendelea na mukutano wa leo. Asanteni sana kwa kufika.

Com. Abida Ali Aroni: Programme ambaye tuko nayo ni inatutaka kufanya mambo mengi na sisi tulifika hapa saa mbili asubuhi na mmeona sasa ni saa sita kasorobo. Tunashukuru watu kama watano ambao wamekuwa hapa kutoka wakati huo, tungependa pia kuwashukuru nyinyi mmekuja, kwa wakati huu tunajua mko na shuguli nyingi lakini nadhania hatutaweza kuanzia programme kama tulivyo tarajia asubuhi na kwa sababu ya muda pengine ningejaribu kwa kifupi tu kuwaeleza mambo mengine halafu tuende kwa draft constitution. Nyote mumepata nakala ambazo zinawaeleza hiyo draft constitution inasema kitu gani.

Kwanza kabisa jiulize ni kwa nini tumefanya mukutano huu na kwa kifupi sana mukutano ambao tuko nao leo kuweza kujadiliana na nyinyi kuhusu hii draft constitution na kuwaeleza kwamba maana muhimu ya sisi kuja hapa ni kutaka tuzungumze ili wakaazi wa sehemu hii na mmesikia tuna Bw. Cllr ambaye atakuja kwenye conference muweze kumtuma na kumwambia yeze na wenzake ambao watatoka District yenu ambao watakuwa ni watu watatu muwaeleze mambo ambayo mungetaka

yapendekezwe katika kikao hicho kikuu cha kitaifa. Ama kama kuna mambo ambayo munaona pengine sio mazuri kwa sababu hii tunaita first draft, sijui kwa Kiswahili first draft nitasema nini lakini, ni tokeo la mwanzo kabisa ya Katiba ambayo inatarajiwa na pengine sio kamilifu pengine kuna mambo ambayo mngetaka kuongeza, kuondoa au kubadilisha. Kwa sababu kama tunavyosema kila siku, Katiba tunayotengeza ni Katiba ya watu wote wa Kenya. Sisi tulikuja tukachukua maoni yenu na tukaketi na kuweza kutoa draft constitution, pengine mumeisoma mkaona ni sawa, au mmesoma mkaona kuna mambo ambayo hamuelewi na mngetaka tufafanue; au mmesoma na mngetaka tubadilishi mambo fulani, sasa hayo ni juu yenu nani lazima mzidi kujadiliana kwa karibu wiki tatu hivi, kwa sababu mkutano huu wa kitaifa unawenza ukafanyika kuanzia tarehe ishirini na nane wa mwezi huu wa kumi. Tumeelewana?

Sasa ndiyo kazi yetu kubwa ni kuangalia sijui ni watu wangapi wameweza hizi nakala kwa sababu zimeweza kuwa zikichapiswa kwa gazette na sisi tumezileta tu ili msiseme kwamba hamjasisoma. Watu wangapi wameweza kusoma au kusikia kuhusu hiyo Draft Constitution? Tuseme ni watu kama nusu, kwa hivyo nadhania tutasaidiana na hao wengine tuweze kupitia kila chapter na kuweza kuona ikiwa kuna kitu hamuelewi tutaelezana kwa kifupi kwa sababu ya muda na mtaendelea kusoma na kuwatuma wakilishi wenu na ikiwezekana muulize vikao tofauti ili muweze kuwatuma wakija kule wakawa wana wakilisha kwa njia iliyo bora.

Na pia kwa sababu matarajio yetu ni kwamba nyote mumawenza kufuata kazi zetu, mnajua kwamba tulikuja tukachukua maoni yenu na sheria ilitulazimu baada ya kuchukua maoni tuweze kuketi na kuweza kuchambua hayo maoni, na kutengeza repoti. Hapo mbeleni tuliwahindi kwamba tutatuma reporti zote katika constituency. Sijui Rose kama uko na hizo repoti katika constituency? Do you have constituency reports with you at the data centre? Katika centre yenu tumeweka views zote tulizopata kutoka sehemu hii na mtaweza kuenda kusoma na mkafanya comparison, na makaratasi ambayo mko nayo. Sasa tuliweza kwa sababu hatukuwa na muda wa kutosha kufanya sampling of views. Tuliweza kuangalia lakini sio kikamilifu tuliweza ku-sample, na tukatoa repoti ambayo kwa wakati huu mumeweza kusoma short version katika gazette. Repoti yetu tumeweza kutoa tafsiri ndogo na ikawekwa katika magazette. Na kwa watu ambao pengine wameweza kufika kwa documentation centre wameweza mmepata vitabu kama hivi ambazo tunaita short version. Lakini ilitolewa tena kwenye gazette, gazette karibu tatu au nne ziliweza kutoa short version, ama toleo fupi ambalo lilieleza jinsi ambavyo tuliweza kufikia draft constitution baada ya kuzunguka na kutembea kote nchini. Na tulipoweza kuchambua kwa kufanya sampling hizo views zenu, tuliweza kukaa na kujadiliana kama Tume ya watu ishirini na tisa, na kujaribu kusikizana ili sisi mwanzo tuweze kusikizana kulingana na vile tulipata maoni yenu, halafu hatimaye ikaandikwa repoti na tukaweza hapo katika hiyo repoti sasa ku-reduce ama kutoa hii report na kutunga sheria. Kwa sababu repoti ni kama hadithi, lakini sheria ni lazima iandikwe kama mnavyona katika makaratasi hayo. Kufikia hapo sijui kama kuna swali kabla hatujaingia katika Draft Bill; kwa sababu siwezi kusema maneno mengi, kitu muhimu kwa vile hatuna muda ni kuangalia hiyo karatasi ambayo mko nayo. Kuna swali lolote kufikia hapo? Nadhania hamna swali kwa sababu hiyo yote ni maelezo. Sindiyo?

Sasa kwa vile mko na Draft Constitution, tunatakiwa tuangalie, chapter by chapter na kuona kama kuna mambo ambayo

mngependa tuzungumzie ama tufafanue ama mkiwa na maswali mtaweza pia kuuliza na kwa uwezo nilio nayo nitawenza kujibu na kutarajia kwamba mtazidi kujadiliana kwa hizo siku ambazo zimembakia kabla ya mkutano mkuu. (interjection) Nafikiri ukiwa na jambo itakubidi uje hapa mbele tafadhali ndiyo tuweze kunasa sauti yako. Na utueleze jina lako na sehemu ambayo umetoka.

Willy Kimeu: Asante sana Madam Commissioner. Mimi naitwa Willy Kimeu. I am a retired civil servant, na kazi yangu I am just a farmer; lakini in most cases huwa na chukuliwa na Electoral Commission naenda kusimamia elections countrywide. Mimi kitu na kuuliza Madam Commissioner, ni assurance zile watu wanajua Kenya hii, Commission yenu tulikuwa tukipata report zingine very negative. Tangu tulipoanza ningetaka utupatie assurance, hakikisho kwamba (1) watu wengine wanesema hii constitution ambayo imekuwa drafted ni ya mtu mmoja. I am sure you know what I am talking about. Na wewe saa hizi umesema mlajadiliana Commissioners 29. Tunataka assurance kwamba wale watu, pengine they are very highly placed Madam Commissioner, hatuko na uoga kwamba there might be an attempt to delay. Hiyo assurance ningependa utupatie kwamba hii report ambayo mmeandika imekubaliwa na Commissioners wale walikubaliwa na bunge yetu. That is one.

Jambo la pili, I am sure you read today's newspaper, Madam, with all due respect, your picture is also appearing there, na hiyo picha inakuja it is trying to associate you with the four Commissioners who are mentioned recently by the Chairman of CKRC, Com. Prof. Yash Pal Ghai when he used some language about some Commissioners who have been undermining the rest of the Commission. I would also seek your assurance Madam, kwamba that problem has since been solved so that we can start. Thank you.

Com. Abida Ali Aroni: Asante Bw. Willy Kimeu. Unajua mtu hawesi kuwa... you cannot judge yourself. Kitu ambacho ningetaka kuwahakikishia mimi kama mtu binafsi ni kwamba mambo ambayo yako kwa gazette leo ni propaganda. Na ni juu yenu nyinyi kama Wakenya kuangalia record ya Macommissioners kwa sababu hata ukisoma gazettee ya leo ya Nation ambayo imesema maneno hayo iko two articles, and the two articles are contradicting. Kwa hivyo usome mwenyewe uone kwamba hiyo ni propaganda ama ni ukweli na uangalie record ya Macommissioners na uone kama ni ukweli. Inasemekana kwamba kuna Macommissioner wanne hawaku-attend launching ya hiki kitabu. Unaona hii kitabu? Na ningetaka ujiulize kama a retired civil servant, kama ukiwa katika kazi na uifanye kwa miaka moja na nusu, halafu siku ambaye watu wa gazette wameitwa ukose kuenda, kama hiyo inamaanisha hukufanya kazi. Hiyo ni PR. Kuunda kitabu kama hiki ni PR sio kufanya kazi. Kufanya kazi ni kule kuenda kuchukua maoni ya wananchi kuchambua na kujadiliana. Sio kukaa katika press conference na mkatokea kwa gazette ama kwa television. So it is up to you to judge. Na kitu ambacho ningewaomba ni kukosa kufuata propaganda za gazette. Na kitu ambacho wewe mwenyewe umesema ni kwamba kuna siasa mingi katika hii kazi yetu ya Constitution Review Commission. Kwa hivyo mimi singependa kuingia katika maneno ya siasa, sitaki kuwa a judge of my own work ikiwa sikuwa nikifanya kazi singekuja hapa kwenu leo. Ningekuja nifike hapa saa mbili? Basi. Nafikiria hiyo ni juu yenu ku-judge na kuacha propaganda, na pia jambo lingine ambalo ningesema ni kwamba, kama Tume tumefikia karibu kikomo cha kazi yetu na kitu ambacho kinambakia ni National Conference na pale katika National Conference, sisi tutakuwa hatuna kazi

muhimu. Kazi muhimu itakuwa inafanywa na delegates na sisi tutakuwa pale kuepeana secretarial support. Kwa hivyo sioni kama Tume ina uwezo wa ku-derail hii shuguli ambayo imebakia.

Na jambo lingine ambalo ni muhimu ni kwamba kwako na kwa wale watu wengine wana haja kuona vile watu wanafanya kazi ni kwamba rekodi zetu zote za Tume ziko wazi na zinatakiwa kuwa katika district documentation centre. Ikiwa Rose hana aende azilete halafu muende muangalie majadiliano ambaye yamekuwa katika mikutano na vikao vya Tume halafu mtaweza nyinyi wenyewe bila propaganda kutambua ni nani ambaye amefanya kazi ambayo ni kulingana na sheria na pia kulingana na matakwa ya wananchi.

Na mwisho kabisa ni kwamba watu ishirini na tisa ambao wametoka sehemu tofauti, wana elimu tofauti, wana background tofauti; itakuwa ni uongo wakiketi na kukubaliana itakuwa ni kama tuna rubber stamp, si ni ukweli? Hata hapa saa hii tukianza majadiliano kila mtu atakuwa na sauti yake, na ikiwa mimi sijakubaliana na wewe, it is wrong kwako kusema nimenunuliwa na KANU ama ni menunuliwa na opposition. Kwa sababu tumekwenda pale kwa sababu ya ujuzi wetu tofauti na misimamo yetu tofauti ya kisiasa, kidini na mambo tofauti ya kijamii. Otherwise hatungekuwa watu ishirini na tisa hasa ukilinganisha na historia ya iliyotupeleka katika CKRC. Sio watu wa musimamo moja na sio watu wa fikira moja. Hiyo ndiyo ningependa kuwaelezea kwa kifupi. Sijui kama nimekujibu lakini nadhania singependa kusema zaidi ya hayo pengine ukiangalia sana undani wa kazi yetu ambayo huwa tuna rekodi mikutano yote utajua ukweli uko wapi na wapi hakuna ukweli nadhania tukiendelea na kazi hii sote tutajua ukweli wa mambo yalivyo. Sawa? Iko swali lingine? Nadhania hakuna. Asanteni.

Sasa katika chapter, pengine tuanze na Preamble. Tulipokuja hapa sehemu yenu na sehemu nyingi nchini, watu wengi walisema wangetaka utangulizi kwa katiba na kwa wakati huu tumetoa utangulizi ambao umeweza kutambua tofauti za kimila, za kidini na pia umetambua umuhimu wa wananchi wa Kenya na kutambua aspirations au sijui tutaita vipi kwa Kiswahili, maadili na hoja ambazo zinazingatia demokrasia sheria na pia uhuru wa mwananchi. Sijui kama kuna mtu ambaye ana tatizo lolote ama ana jambo lolote angeweza kufikiria lakini pengine tutapitia haraka haraka na kujadiliana mwishowe. Katika chapter ya pili, na mnakumbuka chapter yetu ya pili haina Preamble, haina utangulizi, na ndivyo watu wakasema tuwe na utangulizi utakayetutambua na kutambua pia Mwenyezi Mungu katika Katiba ya nchi yetu.

Katika chapter ya kwanza tunazungumza kuhusu wananchi, na sehemu ya wananchi katika utawala wa wananchi na kusema kwamba wananchi ndiyo wenyewe uwezo katika nchi yetu na kwamba uwezo wa wananchi umepewa organs au mikono minne ya serikali. Hapo mwanzoni tulikuwa na mikono mitatu ya serikali na sasa tumeongeza moja. Tuna Parliament ama Bunge, tuko na Koti ama mahakama, na tuna serikali kuu, na wakati huu tumeongeza kuweka Tume ambazo zitakuwa zimewekwa kufanya kazi na Katiba.

Pia tumeangalia umuhimu na ukuu wa Katiba kama sheria muhimu katika nchi na pia tumeangalia Katiba itafunza nini katika nchi yetu; tukasema kwamba itakuza utawala ulio bora itazingatia haki za kibinadamu na pia itatupa nafasi ya kukuza tabia za

kikatiba. Na pia tukangalia jinsi ambavyo mtu akiwa amekosewa chini ya Katiba atafanya aje? Na pia tukataka kwamba kila wakati serikali iwe ina tambua na kuhakikisha kwamba katiba ya nchi yetu imekuzwa. Na tukaangalia sheria ya nchi itakavyokuwa na tukasema kwamba kama ilivyokuwa Katiba ya zamani, ni kwamba Katiba ndiyo sheria kuu na sheria zingine ambazo zinatabulikana zitakuwa chini ya Katiba, na tukasema chini ya ya Katiba tuwe na sheria za kawaida; zile ambazo hutumika katika utawala wa nchi katika kuhukumu watu ambao pengine wamekosa.

Halafu tatu tukasema itakayofuata ni sheria za kitamaduni. Hapo mbeleni katika katiba yetu ya mwanzoni, utamaduni na sheria zetu zilikuwa hazijapewa nafasi kubwa na katika nafasi ya tatu tunaona kwamba tutakuwa na African customary laws. Hapa upande wa ukambani watu walipenda sana kukuza sheria za kitamaduni. Na kumbuka watu walisema watu wanataka ile traditional oath. Simulisema hivyo? Sasa tukaona mambo kama hayo ni muhimu.

Halafu nne tukawa na sheria ambazo ni za Waislamu na jamii ya Kihindu, na pia tukasema tuwe na sheria ambayo inaitwa common law; na pia sheria ambayo ni muhimu ingawa pengine haijaandikwa lakini ukitaka kutekeleza uhaki ni lazima uangalie, tukasema pahali pa sita tuwe na sheria ambayo itatungwa na jamii za nchi ya Africa mashariki, East African Community na hatimaye tuwe na mahali ambapo sheria zitakazokubalika ulimwenguni zinapatiwa nafasi. Kwa wakati huu inasemekana kwamba nchi yetu, au serikali yetu inaweka sahihi kwa mikataba minge ya kidunia, lakini tukifika Kenya haitekelezi sasa Katiba itatulazimu au italazimu serikali kuzingatia sheria hizo za kitaifa.

Halafu tutaangalia chapter ya pili ambayo inazungumzia kuhusu Jamhuri ya Kenya na imetoa principles ambazo ni muhimu katika Jamhuri ya Kenya. Kuna utawala bora kuna multi-party, kuna demokrasia, kuna pia utawala wa kuhusisha mwananchi wa kawaida tunasema kwamba pia tunataka uwazi katika utawala na pia tungetaka separation of powers, ama mikono ile minne ya serikali ipate nafasi ya kufanya kazi yake bila kuingiliana. Na tungetaka pia katika Jamhuri ya Kenya tuzingatie haki za kibinadamu na kuzingatia sheria.

Halafu tunaangalia mipaka ya Kenya. Sitaingilia sana mambo haya kwa sababu kuna mwisho wa karatasi hizo mnazo tumeeleza kwa kirefu sana mipaka ya nchi mtaweza kusoma, na inasemekana Nairobi ndiyo itabaki kama capital city. Tumeangalia lugha za nchi na tukasema Kiswahili na Kiingereza tuwe tunatumia lugha hizo mbili kama official languages. Kwa wakati huu ukienda kama High Court wale ambao wameenda korti kuu hauwezi kuzungumza Kiswahili, ni kweli? Unakuwa na Judge Mwfrika, karani, lawyer Mwfrika wote Waafrika lakini munaambiwa zungumza Kiingereza halafu inatafsiriwa kwa Magistrate kwa sababu Kiingereza ndiyo official language. Lakini sasa inasemekana tutaweza kuzungumza lugha ya Kiswahili official language na pia itakuwa the National language lakini tutakuza lugha zote za makabila yote ya Kenya tofauti ya Kenya na pia tutakuza sign language ambayo inatumika na watu walemavu.

Kuhusu dini imesekana Kenya ni nchi secular. Ni nchi ambayo ina serikali ya kidini na kwamba kutakuwa na serikali na kutakuwa na mambo tofauti ya dini, na kwamba hakuna dini yeoyote ambayo ni official. Dini zote zimebekwa usawa. Nadhania

hayo mengine sio magumu mtaangalia ili tuingie katika chapter tatu ambayo inazungumzia principles au maadili au mambo muhimu katika nchi yetu ya Kenya. Na kwanza tunasema kwamba ni lazima tukuze umoja katika nchi yetu ni lazima tutambue tofauti ambazo zilizoko ili kuweza kukuza utamaduni wa kila jamii katika kila nchi. Tunasema kwamba Kenya kama republic ama Jamhuri lazima izingatie demokrasia, na kuweza kuhusisha wananchi wake katika mambo yote ya utawala. Tunasema pia lazima tuzingatie uwazi katika utawala na serikali ni lazima ifanye juhudzi za kuweza kuondoa rushwa ama corruption katika utawala wa nchi.

Na pia kwamba Jamhuri ya Kenya itapatia mashirika yasio ya kiserikali na vikundi vingine visivyo vya serikali ambazo zinajulikana kwa kimombo kama civil society, nafasi ya kuweza kujihusisha na utawala bora. Mtatambua kwamba hapo mbeleni jambo hilo halikuwa katika katiba ya nchi na tumekuwa na mizozano baina ya serikali na hivyo vikundi visivyo vya serikali. Na kwamba Jamhuri ya Kenya itazingatia kulinda na kukuza haki za kibinadamu; nafikiri mambo mengi hapo yamerudiwa ili kusititiza umuhimu wake katika katiba yetu. Kwamba Jamhuri ya Kenya itakunza ugawanishaji wa rasilimali na maendeleo ya aina yoyote katika sehemu zote za Kenya, na kuzingatia katika ugawanyaji wa rasilimali ya nchi kwamba itaweka maanani welfare ama sijui nitasema aje kwa Kiswahili, umuhimu wa Jamii. Na kwamba Jamhuri ya Kenya itakuwa ni mwanachama mzuri wa wanachama wa nchi za Kiafrika na ulimwengu kwa jumla na kuweza kukuza amani, umoja na ukuzaji wa haki za kibinadamu. Na kwamba kwa kila mwaka hata ikiwa ni kwa mara moja rais wa nchi atatoa repoti kwa Bunge kueleza jinsi Jamhuri ya Kenya imeweza kuzingatia hayo mambo kumi na saba ambayo yako hapa katika repoti ya hii chapter ya pili. Nafikiri mtasoma kwa makini na kuelewa kwa sababu hakuna mambo magumu.

Halafu katika kifungu kumi na tano, tumetoa mambo ambayo mwananchi wa Kenya anapaswa kufanya ama kuzingatia. Katika Katiba yetu ambayo iko kwa wakati huu mwananchi wa kawaida hajapewa duties. Si ni ukweli? Na kwa kawaida tunasikia mwananchi akisema serikali ifanye hivi lakini na sisi sijui tunafanya upande wetu, kwa sababu every duty has an obligation. Si ni ukweli? Sasa hapa tumeweka ili serikali itambue kazi yake na sisi kama wananchi tujue jukumu letu kama wana Kenya ni nini. Kwanza kabisa tunaambiwa kwamba jukumu la mwananchi ni kuelewa katiba ya nchi na kuweza kusambaza maneno ambayo yanatolewa na Katiba.

Pili jukumu la mwananchi ni kuweza kusimama imara na kulinda katiba ya nchi yetu na kwamba ni lazima kila mwananchi aweze kupiga kura na ajihusisha na siasa za nchi. Kwa sababu unaweza wakati mwingine kusikia watu walijiandikisha watu 50,000 kwa kupiga kura na ikifika wakati wa kura unasikia watu 10,000 peke yake ndiyo wamepiga kura, halafu baadaye tunalalamika kwamba hatumpendi mbunge wetu na hatukuenda kumchagua mtu mzuri. Si ni kweli? Hata inasemekana ni jukumu lako kama mwananchi kujitokeza, kujihusisha na siasa, na kuchagua kiongozi ambaye ni mzuri. Si unasema ah ah hiyo kura ni ya watu wale hawana kazi. Kwani watu wengi wale wameandikwa wanaona hiyo ni kazi ya farmers na wale watu wako kwa kijiji. Sasa tunaambiwa ni obligation, ni jukumu lako kama mwananchi kujihusisha na kura na siasa za nchi.

Jambo lingine ni kwamba ni jukumu la mwananchi kufanya kazi, sio kukaa tu kulia lia kwamba mimi ni maskini hivi na hivi na

hutaki kufanya kazi. Na kuweza kujenga nyumba na kusupport family ili tuweze kukuza na kujenga nchi yetu bila kuwa na umasikini. Na pia ni jukumu la kila mwananchi kuweza kujitolea na kuweza kutumia akili yake na uwezo wake katika kukuza nchi na pia ni lazima kila wananchi kujitokeza ila kukuza jamii yake, jamii ni community kwa Kiingereza, na kwamba ni lazima sote kama wananchi kukuza umoja wetu kama Wakenya. Kukuza demokrasia na rule of law, au sheria za nchi. Na pia ni jukumu letu kama wananchi kulinda mali ya umma. Kwa sababu kwa wakati mwangi unaona kama social halls, hospitals, hatujali mambo yake tunaharibu tu kwa sababu tunasema ni mali ya serikali lakini tunasahau kwamba serikali ni sisi. Si ni kweli? Kuna serikali bila wananchi? Hakuna.

Na pia ni jukumu letu ku kuweza kuringa environment na pia kulinda mali ya asili ya nchi, milima mito, forests hiyo ni mali yetu sio mali ya serikali. Kwa hivyo tuna jukumu ya kuweza kulinda ili tuwe na nchi ambayo ni sawa. Na kwamba ni lazima tuweze kushugulika na kuhusiana na watu ambao kazi yao ni kulinda sheria ya nchi, na ni lazima tukose kuhusika na rushwa au corruption na mwisho kabisa tuone jinsi tutaweza kukuza pahali pa Kenya katika ulimwengu mzima. Kwa sababu kwa wakati huu wataalamu wanatwambia jina yetu iko chini sana ulimwenguni. Mnasikia? Sasa hiyo ni jukumu yetu kama wananchi, sio kusema eti hiyo ni kazi ya bunge, tuone tutakuza sehemu yetu kivipi katika jamii ya ulimwengu.

Chapter ya nne ni kuhusu uraia. Ni nadhania hapa nita summarize kwa sababu hakuna mambo magumu. Kwanza kabisa article ama kifungu kumi na sita inasema kwamba, kila mwananchi ana haki sawa. Hakuna mwagine important ama muhimu kuliko wenzake, na kama kuna mapato, privileges ye yeyote kutoka kwa serikali iwe inafanyiwa usawa kwa wananchi wote. Na kwamba sisi wote tuna rights and duties. Tunapewa uhaki sawa na kwamba kila mwananchi wa Kenya apate nafasi ya kupata passport, identity card, birth certificate na document ye yeyote ambayo inatolewa na serikali kwa usawa bila ubaguzi.

Halafu zingine zinatwambia mtu atakuwa mwananchi wa Kenya ki vipi kupitia kuzaliwa Kenya, kujandikisha, halafu pia tunaambiwa kwamba mtoto ye yeyote anayezaliwa na mwananchi wa Kenya awe baba ndiye Mkenya ama mama atakuwa mwananchi wa Kenya, sheria ya wakati huu inasema ikiwa baba sio Mkenya wewe sio Mkenya. Lakini akina mama walilia sana na watu ambao hawapendi ubaguzi akina baba wakasema kweli hiyo sheria ni mbaya na tukasikia. Sasa msichana wako hata akizaa na mzungu mtoto anakuwa Mkenya sio lazima amulete Mzungu hapa kuwa Mkenya. Na pia mtu ambaye ni mwanaKenya kulingana na sheria hawezikunyang'anywa uraia bila kupitia haki ambazo zimebekwa katika katiba.

Jambo lingine ni kwamba, mtoto ye yeyote ambaye ana umri wa miaka chini ya minane amepatikana Kenya na wazazi wake hawajulikani atatabulika kama mwananchi wa Kenya. Na hii ni kwa sababu tuna hii watoto wako katika mabara bara wakati mwagine ukiuliza baba ni nani hawajui, kwenu ni wapi, Nairobi; mama ako wapi alikufa. Sasa hujui kwao ni wapi, na wanazungumza lugha inayoitwa sheng. Sasa hata huwezi kujua kama ni Mkamba ama ni kabilia gani. Sasa inajulikana watoto kama hao wote watatambulika kama wananchi wa Kenya.

Halafu katika sheria ya wakati huu, tulikuwa hatuwezi kuwa na uraia wa nchi mbili Katiba ya wakati huu inasema kwamba

mwananchi wa Kenya anaweza kuwa na uraia wa nchi mbili. Mengine mtasoma na inasemekana kwamba Bunge itatengeza sheria ambazo zitasaidia utekelezaji wa mambo ambayo yako katika Katiba kuhusikana na uraia.

Chapter ya tano ambayo ni muhimu zaidi ina zungumza haki za kibinadamu – the Bill of Rights, na pengine hapa mungetaka kuwa waangalifu zaidi, na inasemekana kwamba haki hizi za kimsingi ni haki ambazo ni lazima kila Mkenya apewe na serikali. Na kwamba mtu hawezi kunyang’anywa hizi haki za kimsingi ila kwa kifungu kingine cha kikatiba. Kama katiba haija kunyima haki yako ya kimsingi hakuna sheria au mtu yeoyote ambaye anaweza kukunyang’anya. Na pia serikali ikapewa jukumu ya kuhakikisha ya kwamba hizi haki za kibinadamu zinafuatwa. Imesemekana serikali lazima itunge sheria ambazo zitaambatana na haki za kibinadamu. Lazima iwe na policy au utaratibu wa kazi zake ambazo **zitazingatia** haki za kibinadamu, na katika kazi zake za utawala ni lazima serikali izingatie haki za kibinadamu.

Na kwamba parliament itaweza kuweka tume ambayo itazingatia na kuhakikisha kwamba haki za kibinadamu zinafuatwa. Na kwamba nchi ya Kenya itaweza kuzingatia maagano ambayo ni ya kiulimwengu ama ya meandikishwa na nchi za kiulimwengu kulingana na haki za kibinadamu. Halafu tukaambiwa kwamba ingawa tuko na hizo haki, lazima hizo haki zipunguzwe wakati mwingine. Limitation of rights. Na tukaambiwa hata ikiwa umepewa haki, wakati mwingine sheria inaweza kukunyima haki hiyo; na hiyo haki ambayo unaweza kunyimwa ni lazima iwe ni ya halali au umenyimwa kwa njia halali, njia ambayo itazingatia demokrasia, itaangalia usawa na lazima iangaliwe ni kitu gani ambacho unanyimwa, umuhimu wa hicho kitu na pia.... **end of side 1A** freedom ambayo haina kiwango. Kwa mfano tuchukue freedom of worship. Watu ambao wamesoma wataona Katiba hii hata imetupatia freedom of worship zaidi hata kushinda ile ingine. Na hapa Kenya tunasema hatutaki watu ambao wana abudu shetani. Sindio? Ingawa una freedom of worship ukitaka kuabudu shetani ni kufanya mambo mabaya unaweza kukatazwa na ukaambiwa sababu ingawa katiba inakuambia una uhuru wa kuabudu unakatazwa kwa sababu mambo hayo haizingatii katiba yetu haizingatii haki za kibinadamu ha mambo kama hayo. Tumelewana? Huo ni mfano mmoja tu.

Halafu kifungu cha thelathini na mbili, tunaambiwa kila mwananchi ana haki ya maisha. Na kwamba hukumu ya kifo imeondolewa na kwamba pia kifungu cha thelathini na tatu kila mwananchi ni sawa mbele ya sheria, na sheria itaweza kuzingatia sisi wote na kutupatia manufaa kwa usawa. Hakuna mtu ambaye ni muhimu kuliko mwingine mbele ya sheria.

Kifungu cha tatu tumepatiwa uhuru wa kukosa kubaguliwa. Na ikatolewa mifano na tukaambiwa sote tutakuwa ni sawa bila kubaguliwa kupitia rangi, maumbile, akina mama ambao ni waja wazito, au watu ambao hawajaolewa wakati mwingine unaskia huyu mama hajaolewa kwa hivyo hawezi kupata hii cheo kwa sasa inasemekana mtu asibaguliwe kwa sababu ya status yake katika society. Usibaguliwe kwa sababu ya kabilia lako, usibaguliwe kwa sababu ya umri wako, dini au kwa sababu wewe ni mtu mlemavu au kwa sababu ya lugha unayotumia, au mafikirio yako.

Halafu kifungu thelathini na tatu kinazungumzia kuhusu akina mama, na inasemekana kwamba akina mama wana uhaki sawa na wanaume; na pia wapatiwe nafasi sawa na wanaume katika siasa, uchumi na mambo ya kijamii. Sasa hiyo sijui wazee

watasema aje lakini wakati wa kujadiliana mtatuambia. Na pia kwamba mama wapewe heshima sawa na wanaume. Akina mama na wanaume wawe na haki sawa ya kuweza kurithi mali, kupata nafasi ya kufikia na kuweza kuwa na kumiliki mali. Na kwamba sheria yoyote isitumike kubagua akina mama, iwe ni sheria za kitamaduni; na kwamba serikali inapewa jukumu ya kuhakikisha kwamba imewachunga akina mama na haki zao, na kutambua nafasi ya akina mama katika jamii yetu kama watu wa Kenya. Pahali pa akina mama sio kusemekana ni jiko kwa hivyo wasahaulikane. Serikali itambue hata kuwa jikoni ni kazi. Na pia akina mama wapewe nafasi na vifaa vitakavyoweza kuwapatia nafasi ya kujiendelesha.

Kifungu thelathini na tisa kinazungumza kuhusu watu wazee. Watu ambao wamestaafu ni watu wazima, na tuliambiwa kwamba wamesahaulika serikali imewasahau na wengine imewabidi waende kwa nyumba ya wazee. Sasa tunaambiwa kwamba hawa wazee ni lazima watambulikane kwa vile nafasi ya kujihusisha na shuguli za kitaifa, wapewe nafasi ya kukuza mambo yao, wasimbaguliwe na kutukanwa; na wapewe heshima ambayo inafaa kupewa watu wazima. Na kwamba ni jukumu la serikali na jamii ya watu hawa kuwalinda na kuhakikisha kwamba hawana shida yoyote.

Halafu kifungu thelathini na saba kinazungumza kuhusu watoto na kutambua sehemu ya watoto katika jamii na haki za watoto. Kwa sababu katika katiba ya wakati ambayo tunayo sasa haijatambua haki za watoto, na tunaambiwa kwamba watoto wote waliozaliwa nje ya ndoa wapewe haki zilizo sawa, sijui mtasema aje, mtatueleza. Na kwamba haki ya mtoto na masilahi yake ndiyo yatatiliwa mkazo katika mambo yoyote yanayohusisha mtoto. Na kwamba wazazi wote wawili ikiwa wameoana na hawajaoana ni lazima wazingatie mambo ambayo ni muhimu, ya mtoto na kumlinda. Na tumepewa mambo mengi hapa ambayo. Ni muhimu kwamba kila mtoto ni lazima apate jina la kifamilia na kuwa na uraia wa nchi fulani ni lazima akingwe na wazazi wake, ni lazima apate masomo ya bure na ya lazima. Ni lazima achungwe ili asipatikane na madhara kupitia mambo ambayo ni ya kitamaduni, cultural rights na practices. Na ni lazima huyo mtoto akingwe ili wazazi wake wasimtupe na kukosa kumuangalia. Lazima mtoto apate chakula cha kutosha, na apate matibabu. Na kwamba watoto wasiadhibiwe kwa kupewa adabu ambayo ni kali, corporal punishment, ama ambayo pengine ni kinyume cha haki za kibinadamu. Na pia mtoto asishikwe na kuweka gerezani, ila ikiwa ni lazima na ikiwa ni muhimu kwa maisha ya huyo mtoto na ikiwa mtoto ameshikwa ni lazima ashikwe kwa muda mfupi zaidi na akiwekwa gerezani asiwekwe na watu wazima. Na ni lazima serikali impatie wakili wa kuweza kumteteta ikiwa atapelekwa mahakamani. Na kwamba watoto ambao ni walemaru wawe ni wasichana, yatima wasio na mama na baba, watoto refugee, waweze kuangaliwa kikamilifu na serikali. Na kwamba kwa sasa mtoto ametabulika ni ule ako chini ya miaka kumi na nane.

Halafu tumezungumza kuhusu family. Katiba ya wakati huu haituelezi familia ni nani na nini kinatakikana katika family na inasemekana kwamba familia ni msingi katika jamii yoyote. Na kwamba mtu atakayefikisha miaka kumi na minane ana haki ya kuolewa ama kuoa, ana haki ya kuanshiza familia na kwamba bibi na bwana katika familia wana haki sawa sawa.

Kifungu cha thelathini na tatu kinazungumza kuhusu watu ambao ni walemaru na katika sheria wakati huu walisahaulika kwa hivyo tumetoa na kusema wanafaa kuwa na haki kama wakenya wengine, wanafaa kupekekwa shule. Wanafaa kupewa

mafunzo ambayo yatawafaa, na pia ni lazima serikali ihakikishe ya kwamba wanaweza kufika sehemu zote bila pingamizi katika public transport. Waweze kupewa vile wataweza kupanda basi, katika gorofa wapewe vile wanaweza kupanda hizo gorofa; ili wasiweze kukosa huduma kwa sababu ya hali yao. Na ni lazima tutumie sign language ili mtu aweze kuelewa mambo yanayoendelea, na pia wahuishwe katika utawala wa nchi na wapate usaidizi unaofaa kulingana na hali yao.

Halafu katika kifungu arobaini tunaongea kuhusu human dignity ama heshima ambayo kila binadamu anafaa kuwa nayo. Halafu tunaangalia freedom and security kwamba tuna haki na ni lazima tulindwe na serikali. Kifungu arobaine na mbili kwamba ni lazima Mkenya yote asifanywe mtumwa, na asilazimishwe kufanya kazi.

Halafu tunaangalia privacy, na inasema kwamba mtu ye yeyote asifanyiwe msako kwa nyumba yake na vitu vyake au na mali yake, ila kwa njia iliyohalali. Na kwamba mtu ye yeyote asilazimishwe kutoa siri ya jamii yake.

Halafu katika kifungu arobaini na nane, kuna haki ya kuabudu na tuanambiwa ya kwamba kila mwana Kenya ana haki ya kuabudu, kufikiria na kuwa na opinion, sijui opinion nitasema nini nimesahau kidogo – maoni. Uwe na fikira, maoni na dini utakayo taka. Na unaweza kujumuika peke yako na jamii au na kikundi cha watu katika kuabudu, kufundisha ama kufanya mambo ambayo yanatakikana katika dini au mambo unayofikiria. Ndiyo ni kasema kama hiki kifungu wakati mwingine utaambiwa ah ah sorry sasa hapa kuna limitation. Simunaona? Kwa sababu inatupatia nafasi ya mambo mengi. Pia tumeambiwa kwamba, kila jamii ya kidini itaweza kuanzisha sehemu yake ya kuabundu na shule bila pingamizi. Na kwamba tukiwa na shuguli za Kitaifa dini zote zitatabulika na kupewa nafasi sawa.

Kifungu kingine kinasema kwamba Mkenya asilazimishwe kufanya jambo lolote ambalo litakuwa ni kinyume cha dini yake. Halafu kuna freedom of expression, tunaambiwa kwamba tuwe na uhuru wa kuzungumza, na tukapewa hapa vifungu nne ya kuonyesha uhuru ambao tutakuwa nao; lakini tukaambiwa hiyo uhuru pia isipitishe kiwango na tunaabiwa hiyo uhuru isitoe porojo ama propaganda na pia isiweze kuwesheza wananchi kufanya vita ama kuleta vita, ama watu kuchukiana katika jamii.

Na pia tunaambiwa tutaweza kuwa na uhuru wa kuchapisha na kuandika kupitia magazetini, radio na television. Na kwamba kifungu cha arobaini na saba kila mwananchi ana haki ya kupata maneno ambayo ni ya kiserikali. Halafu tumepewaa haki ya freedom of association. Watu wanaweza kukutana bila pingamizi, unaweza kujiunga na kikundi chochote bila kulazimishwa; na kwamba serikali isikatae kuandikisha kikundi chochote ambacho kisicho cha serikali ila kwa sababu muhimu. Na kwamba ikiwa kuna malipo serikali isitoze malipo ambayo ni mengi.

Halafu tumepewaa haki za kisiasa. Kwamba kila mwananchi ana haki ya kujiunga ama kuanzisha chama cha kisiasa. Kila mwananchi ana haki ya kujumuika na shuguli ya chama cha kisiasa. Na kila mwananchi ana haki ya kufanya campaign ya chama chake. Na kwamba kila mwanakenya apate nafasi ya kufanya uchaguzi wa haki na wa halali. Na kwamba kila Mkenya ambaye amefikisha umri wa miaka kumi na minane ana haki ya kujandikisha na ya kupiga kura ambayo ni ya siri.

Halafu tumepatiwa haki pia ya kuweza kutembea na kuishi pahali popote Kenya, halafu pia tumeangalia haki ya watu ambaeo ni wakimbizi. Katiba imesema kwamba, mtu atakaetambulikana kwamba ni mkimbizi atapewa haki fulani na kwamba parliament itaweza kutoa sheria itakayoweza kuchunga masilahi ya hawa watu. Tumepewa pia haki ya kuweza kufanya biashara, kujishughulisha na kazi ambayo mtu atataka kufanya bila kuwa na ubaguzi wowote. Kifungu arobaine na nane kinazungumza kuhusu mali na jinsi ambavyo kila Mkenya ana haki ya kununua na kua na mali, either akiwa peke yake ama akiwa na kikundi cha watu.

Na kwamba bunge itatengeza sheria ya kulinda mali hizo. Halafu tunaangalia haki za wafanyi kazi na kwa wakati huu mnasikia vile zinavuma. Sheria inasema kwamba kila Mkenya ana haki ya kupewa maslahi mahali ambapo wanafanya kazi ni lazima alipwe ujira unaofaa, ama mshahara unaofaa. Ni lazima apataiwe haki fulani ambazo zinafaa kufanya kazi yake, na pia kila Mkenya ambaye ni mfanyi kazi ana haki ya kujiunga na chama chochote cha wafanyi kazi, na pia ana haki ya mgomo. Lakini sasa hiyo sheria hiyo ni sheria ambayo itakuja – mkikubali huko katika National Conference.

Pia tunaambiwa waajiri wana haki, na wanahaki ya kujiunga na vyama vyaa waajiri na kujihushisha na shuguli ya vyama hivyo. Na kwamba vyama vyaa wafanyi kazi na vyama vyaa uwajiri zitakuwa na shuguli zake bila pingamizi; vitawea kutekeleza kazi yake bila kuingiliwa.

Halafu tunaingilia social security, haki za kijamii na tunaambiwa kwamba ikiwa kuna watu ambaeo hawajiwezi kabisa; itakuwa ni jukumu la serikali kuwangalia. Na upande wa matibabu kwamba kila Mkenya ana haki ya tiba na hii haki ni pamoja na haki yakujishughulisha na uzazi. Na hakuna mtu atakaenyimwa matibatu wakati ambapo anadharura ama emergency. Kwa sababu wakati mwengine watu wanaenda emergency na wananyimwa hata Kenyatta unaambiwa kama sijui hulipi pesa ngapi huwezi kutibiwa. Sasa katiba inasema ikiwa mtu ni mgonjwa sana, amaako katika hali ya hatari lazima apatiwe matibabu kwanza.

Elimu – kifungu hamsini na nane, kwamba kila Mkenya ana haki ya elimu ya kimsingi ikiwa ni shule ya nursery, primary na secondary. Na kwamba serikali itaaniszisha mpango utakaohakikisha kwamba kila mtoto anapata elimu ya bure na ya lazima katika shule za msingi. Na kwamba serikali itahakikisha kwamba kuna utaratibu unaofaa wa kutekeleza na kuendesha elimu, baada ya elimu ya shule ya upili. Na kwamba mtu yeoyote ana haki kulingana na sheria kuanshiza shule ama taasisi elimu.

Nyumba- kifungu hamsini na sita, kwamba kila Mkenya ana haki ya kuishi katika nyumba iliyo bora. Sasa hapo sijui nyumba iliyo bora ni gani, lakini nina hakika watu wakijadiliana watu watajua. Na kwamba Mkenya asifukuzwe katika nyumba anayoishi, wala isimbomolewe ila kwa kupitia katika order itakayotolewa na korti. Na hiyo korti inafaa kusikiza maneno kwa makini na kutoa amri hiyo kulingana na sheria, na mambo ambayo yanafaa. Na kwamba bunge itatoa sheria zitakazohakikisha mambo haya.

Upande wa chakula kwamba tuna haki ya kukosa kuwa na njaa, na ni lazima tupate chakula kizuri na cha kutosha. Kila Mkenya anafaa kupata maji masafi na maji ya kutosha. Na pia tumezungumza kuhusu usafi na tunasema kwamba ni lazima wakenya wote wahakikishe usafi, na katika usafi huo tunasema pia kuhusu tabia za kuzika watu na pia tunasema ni lazima watu ambaa wamefariki wazikwe kwa njia ya usafi na ya heshima. Halafu tunaingilia environment, mazingara; na tunasema kwamba kila Mkenya ana haki ya kuishi katika pahali ambapo ni pazuri, ni sawa kwa maisha yake, na kwamba kila Mkenya ana haki ya kuchunga sehemu ambayo anaishi ili kuhakikisha ya kwamba tunaweza kukosa kuwa na hewa mbaya, tutaweza kufanya conservation na kuchunga mambo ambayo yatakosa kutupatia madhara ya kiuchumi na ya kijamii. Na kwamba kila Mkenya ni lazima apate information au habari kuhusu mazingara.

Halafu tumepewa haki ya wanunuzi, haki ya watu ambaa wanakwenda na kununua services, ama vifaa. Na tunaambiwa kwamba vitu, - na kwa wakati huu Kenya hata ukienda ununue sharti ambayo imepasuka sio hatia, si saa ingine unanunua unapata kiraka? Na nguo imefungwa kwa karatasi, sasa tunaambiwa vitu ambavyo tunanunua, huduma tunazopata ni lazima ziwe za hali ya juu. Sasa hiyo ni sheria. Na kwamba ni lazima tupewe information au habari zitakazowesheza mtu kujua manufaa ya huduma ama kitu ambacho unanunua. Na kwamba ukinunua kitu chochote ama kupewa huduma ni lazima ikinge afya yako na pia iangalie masilahi yako ya kiuchumi. Na kama kuna huduma ama kitu ambacho umenunua ambacho ni kibovu na kimekupatia hasara, au madhara yoyote ni lazima ulipwe gharama yako na loss ambayo utakuwa umepata. Kama umeumia hasara ile umepata. Na kwamba watu ambaa watakuwa wakiiza ama kutoa vifaa ni lazima wajihushishe na vyama ambavyo ni vya watu kama hao, ili waweze kutekeleza mambo ambayo yamesemekana.

Halafu kifungu sitini na sita ni kwamba Mkenya hana ruhusa ya kukubali kufanya jambo ambalo ni kinyume na sheria. Na kwamba kila Mkenya ambaye ana jambo ambalo angependa kupeleka kwa korti aweze kupatiwa nafasi kortini na kusikizwa kwa njia ya haki na halali. Na kwamba ikiwa umeshikwa kwa kudhaniwa kwamba umefanya kosa unahaki ya kunyamaza sio kupigwa na kulazimishwa kuongea. Pia ni lazima uelezwe kosa lako kwa lugha ambayo unaelewa; na ukishikwa na polisi wakueleze kwamba unaweza kuzungumza ama kunyamaza. Sio ukifika unaambiwa andika statement. Na pia si lazima ulazimishwe kufanya confession – kusema siri yako. Unajua wakati mwengine unashikwa na unaambiwa sasa ni lazima useme ama kama husemi utafanya hivi na hivi na unasema mambo ambayo pengine yatakudhuru baadaye. Sasa inasemekana ukifanya hiyo confession ambayo inaweza kutumiwa baadaye ikakudhuru na ukitaka ku kutoa hiyo confession utoe ukiwa umependa mwenywewe. Na ikiwa umewekwa remand, usiwekwae na watu ambaa wamefungwa. Na ukishikwa ni lazima upelekwe korti halaka iwezekanavyo na isipite masaa arobaine na manane. Na ikiwa umeshikwa pahali mbali sana na korti wajaribu haraka iwezekanavyo kukupeleka kwa korti; na ukifika kortini mara ya kwanza ni lazima uelezwe makosa yako na korti na upewe bond ya kutoka ila ikiwa sheria imekataa, na ikiwa umefanya kosa na kuhukumiwa. Ikiwa kosa hilo linaweza kulipa fine na chini ya miezi sita usifungwe.

Na pia kifungu ishirini na tisa kinaongea jinsi mtu atapewa haki katika mahakama kwa kusikizwa kwa njia iliyo bora, nafikiri hayo ni mambo ya kawaida mtasoma tu kwamba mtu akishikwa asidhaniwe ni mhaliu bila kusikizwa na korti na kusemekana

kwamba amepatikana na hatia aelezwe makosa yake apatiwe wakati wa kutosha wa kuweza kujitetea. Kesi ifanywe wazi wazi sio chambers, ifanywe open court, na isichelewe ifanywe haraka iwezekanavyo na usifanyiwe kesi yako ikiwa hauko pale, na upewe nafasi ya kuchagua wakili wako. Na ikiwa unakosa pengine ukihukumiwa itakuwa na kifungo cha juu zaidi, serikali ikupatie lawyer ama wakiri. Na pia una haki ya kunyamaza bila kuzungumza katika korti, na unahaki ya kutoa ushahidi, na pia ni lazima upewe interpreter ikiwa hauelewi lughya ya korti, na pia upewe haki ya rufani. Halafu tumepewa haki za watu ambao wameshikwa na kuwekwa custody ama wamefungiwa.

Kifungu sabini na moja tunaelezwa ni wakati gani ambapo nchi inaweza kuwa katika hali ya hatari, state of emergency. Na tunaambiwa ni wakati tu ambapo kuna vita ama tumeingiliwa, ama kuna shida ambayo haikuweza kuepukikana, ama kuna jambo la dharura. Na pia baada ya mambo hayo kuisha ni lazima kufanywe matangazo ya kusema kwamba hali hiyo imeondolewa. Na kwamba kutangazwa kwa hali hiyo ni lazima majadiliano yafanywe katika bunge. Na kwamba hali kama hiyo isizidi miezi miwili. Kifungu ishirini na mbili kinaleza jinsi ambavyo mtu atawezekuha kuhakikisha kwamba haki za kimsingi zinafuatwa na hiyo imeendelea mpaka kifungu sabini na tano, na fikiri hapo mtawezekuha kusoma kwa sababu tumezazungumza mambo ya haki za kimsingi.

Chapter ya sita tunazungumza kuhusu electoral system and process, au kwa njia nyingine tunasema jinsi ya uwakilishaji. Na tunaambiwa kwamba hiyo electoral system itakuwepo wakati ambapo wananchi tutaweza kusimama kwa kura na kwa kuchaguana na kuchaguliwa; ni lazima kura iwe ya siri, ni lazima iwe ya halali na kwamba ni lazima kura zifanywe kwa njia iliyo bora, na lazima akina mama, watu walemvu na makundi ambayo ni madogo yataweza kuhusishwa. Na kwamba kura itawezekuha kusimamiwa na kikundi ambacho kimejisimamia na hakijaingiliwa na siasa za upande wowote.

Na kifungu cha sabini na saba kinatueleza jinsi ambavyo bunge litaweza kuendesha mambo hayo. Kifungu sabini na nane kinatueleza vile mtu yejote ambaye ana miaka kumi na nane na zaidi ana haki ya kupiga kura, na kwamba hakuna kitu chochote ambacho ni cha kiserikali kitazuia mtu kupiga kura, kusimama wakati wa kura, na pia tunaelezwa ni akina nani wanaweza kuandikishwa kupiga kura. Tunaambiwa ni mtu wa miaka kumi na minane, ni mtu ambaye kawaida anaishi nchi ya Kenya na ameishi hapa zaidi ya mwaka mmoja. Kuna masharti mengine yameandikwa hapa, na kwamba mtu atawezekuha kuiandikishwa hapa sehemu moja peke yake.

Halafu tunaelezwa jinsi mtu atakatazwa kuiandikishwa. Tunaambiwa mtu ambaye hana akili sawa sawa, mtu ambaye ameshitakiwa na akasemekana kwamba amefanya makosa kulingana na sheria za kupiga kura. Na ikiwa kuna tashwishi mambo hayo yatapelekwa high court na yatatatuliwa. Halafu tunaambiwa tume ya upigaji kura tunahakikisha kwamba upigaji kura umerahisishwa. Kwamba watahakikisha box za kura zinaonekana ndani sio nyeusi, transparent. Ukiangalia unaona kura ngapi zimeingia na kwamba kura zitakazopigwa zitahesabiwa na kutangazwa katika polling station ambako kura imepigwa. Na ikiwa kuna mtu amesimama na hakupingwa basi atatabulika kwamba ndiye mshindi ama ndiye amechaguliwa.

Halafu kifungu themanini na tatu kina tueleza kuhusu Electoral Commission. Kwa wakati huu tuna macommissioner ishirini na wawili katika tume hiyo, na sasa inasemekana kwamba kutakuwa na mwenye kiti na macommissioner wasiopungua nane na kuzidi kumi. Tunapendekeza kwamba wapunguzwe na sasa hapa pengine tunapendekeza vile watakavyo fanya kazi yao; na kwamba Commissioner wa Tume hiyo asiwe ni Mbunge na asiwe na shughuli zingine za kitaifa.

Kifungu thamanini na nne tunaeleza kazi ya Tume hiyo na mtaona kazi yake imeongezeka. Wanaambiwa kwamba watafanya continuous voter registration, sasa tutukuwa tunajiandikisha wakati wowote kwa sababu tunajua watu wanafikisha umri wa miaka kumi na minane kila wakati. Na kwamba watatazama shuguli za constituency na pia wataweza kusimamia kupiga kura; watahakikisha kwamba ni za haki na za halali. Watafanya supervision na kusimamia vyama vy'a kisiasa, na watafanya management ama watasimamia fedha ambazo **end of tape 1**.

Tape 2

Kwa election na wanafunza wananchi elimu ya kupiga kura na demokrasia, na watajaribu ku-monitor ama kufuata ama kuhakisha kwamba kazi ya kupiga kura inafanywa ki sawa sawa. Na kwamba watakuwa ni tume huru.

Halafu kifungu thamanini na saba tunazungumza kuhusu vyama via kisiasa, na pia inasemekana kwamba vyama vy'a kisiasa vitapatiwa pesa na serikali kulingana na sheria itakayotungwa na parliament. Na hapa tunapewa kazi ya vyama vy'a kisiasa kwa sababu hatukujua ama mlikuwa mnajua kazi yake? Kupiga kura na propaganda, mlikuwa mnajua? Sasa tumeambiwa hapo kwamba kazi yao itakuwa ni kukusanya wananchi na kuwaeleza mambo ambayo ni ya kitaifa na yatakayoweza kutuweka pamoja kama wananchi wa Kenya, na pia itaweza kukusanya watu ambao wako na fikira sawa kuwa pamoja, na itaweza kuwaeleza watu kuhusu mambo ya kisiasa na kikatiba na haki za kibinadamu, na haki zingine hata na haki za kisiasa. Na pia kukiwa na shida baina ya vikundi visivyo vy'a serikali na kisiasa zitajaribu kusaidia, na kwamba kitaweza kutupatia kama wananchi nafasi tofauti ya kiuchumi, ya kisiasa na ya kijamii kupitia kwa kura.

Na pia wataweza kuangalia kwamba kuna umoja na kuna nidhamu katika serikali, na kwamba vitaweza kuhakikisha ya kwamba serikali iko wazi kwa bunge na wananchi. Na sasa pia inasemekana kwamba Electoral Commission ndiyo itakuwa inaandikisha vyama vy'a kisiasa. Na tukaelezwa jinsi watakavyofanya kazi hiyo, na jinsi watakaweza ku-register ama ku-cancel political parties.

Kifungu cha tisaini na tatu tunaelezwa kuhusu pesa za vyama vy'a kisiasa na tunaambiwa kwamba kutakuwa na fund itakayoitwa political parties fund. Na kwamba hiyo fund itashugulikiwa na tume ya Electoral Commission. Na tukaelezwa pale pesa hizo zitatoka. Hizo pesa zitatoka kwa serikali kupitia bunge na isizidi 0.3% ya budget ya nchi yetu katika kila mwaka. Na pia Tume hiyo inaweza kupata misaada kutoka mashirika mbali mbali na watu mbali mbali.

Halafu tunaelezwa kazi ya pesa hizo ambazo zinasemekana ni pesa za kisiasa tunaambiwa pesa hizo zitashughulikia mambo ya election, uchaguzi. Zitasaidia vyama vya kisiasa kutoa elimu ya raia kuhusu demokrasia na mambo ya kupiga kura na asilimia 10% ya pesa zitakazotolewa chama chochote chini ya asilimia kumi ya pesa hizo zinaweza kutumika kwa kushughulikia mambo ya vyama hivyo. Kama mishahara, rent na vitu vya kawaida vya vikundi. Na tunaambiwa kwamba chama chochote kikipatiwa pesa visitoe pesa hizo kwa njia yoyote kama zawadi, hata mishahara hawawezi, ama kupatia mtu wowote member ama supporter wa hiyo party pesa hizo. Na pia wasitumie kwa njia yeyote ambayo itakuwa ni kinyume na ukuzaji wa demokrasia ya vyama vingi.

Na kwamba hiyo pesa tumeambiwa ni 0.3% nusu yake itagawanyishwa kwa usawa kwa vyama ambavyo vilipata asilimia tano ya watu waliopiga kura nchini. Kwa hivyo sio vyama vyote lazima chama kitachofaidika kiwe kilipata at least 5% of the total votes. Na pia asilimia hamsini itakayo mbaki itatolewa kulingana na kura ambazo vyama tofauti vilipata. Chama ambacho kilipata kura nyingi kitapata zaidi hivyo hivyo mpaka wafikie chini. Mmeelewa?

Halafu tumeambiwa kwamba Electoral Commission ita supervise parties, na tukaelezwa vile itafanya kazi, na tukaambiwa lazima kuwe na discipline katika party, na tukaelezwa hiyo discipline itakuwa ya aina gani. Na tukaelezwa pia katika kifungu mia, rais wa nchi mtu wowote ambaye ana ofisi ya kiserikali juu ya deputy secretary, asiwe na cheo katika chama cha kisiasa.

Halafu tunaingia Parliament (interjection: sasa tufanye hivi ukiwa una swali ui-keep saa ile tunaendelea ndiyo ni ifafanue. Sawa?) Tunaangalia bunge, tunaambiwa kwamba kwa wakati huu tutakuwa na bunge ambayo itakuwa mara mbili. Kutakuwa na National Assembly, na ingine inaitwa National Council. Wakati huu tuna bunge moja lakini tunaambiwa itagawanyishwa mara mbili. Na tunesema kazi ya bunge tunaambiwa bunge ni lazima ihakikishe ya kwamba ina watu ambao wana wakilisha watu tofauti, yaani makabila tofauti na watu tofauti na shuguli ya bunge itakuwa kuandika sheria, kujadiliana na kutoa maagizo muhimu. Na kwamba itatupatia sisi kama wananchi nafasi ya kuweza kujadiliana mambo ambayo ni muhimu katika nchi yetu. Bunge itaweza kuitisha pesa zitakazoweza kutumika katika serikali. Bunge pia itaweza kufanya mabadiliko ya kikatiba kulingana na chapter kumi na nane. Utaona vile tumeambiwa, na pia kwamba itaangalia shuguli za serikali na pia itaangalia na kuitisha international treaties; au magano ambayo yanafanywa huko katika mikutano ya ulimwengu, na pia itakagua mambo yanayofuata ambayo yanafanywa na President. Kwa mfano watu ambao Rais atataka kuchagua waingje katika cabinet wataweza kukataa ama kukubali, watu wengine ambao President atakua amechagua na pia wataangalia conduct ama tabia ama mambo inafanywa na watu hao, Rais, makamu wa Rais, Prime Minister, Ministers, wafanyi kazi wa mahakama na wafanyi kazi wa ofisi za kiserikali na pia itaangalia na kukubali wakati ambapo tutaweza kutangaziwa hali ya hatari.

Na kwamba Parliament itakinga na kukuza katiba ya nchi na kuweza kuhakikisha ya kwamba kuna utawala wa kidemokrasia. Na tukaambiwa kwamba ukiangalia kifungu cha mia moja na tatu kwamba parliament italazimika ku-approve ama kukumbaliana na appointment za watu wafuatao. Watu ambao watakuwa katika Judicial Service Commission, au tuseme watu ambao watakuwa katika Tume za kikatiba wote, Mkuu wa Sheria, atakaesimamia kesi za serikali, Ombudsman au public

defender, Commissioner wa Polisi, Majudge na Chief Kadhi, na hiyo itafanywa na sehemu ya bunge inayoitwa National Council na tutakuja kuona National Council ni watu gani, na National Assembly ni watu gani.

Nayo National Assembly itatambua na kukubali watu wafuatao, Prime Minister, deputy Prime Minister, Minister, deputy Minister, Permanent Secretary, Ambassadors, Electoral Commission, Mkaguzi wa fedha za umma, Director of Central Bureau Statistics na Governor wa Banki kuu ya Kenya. Kwa hivyo hizo nyumba mbili za bunge zitakuwa na kazi mbili tofauti.

Na sasa tunaelezewa kifungu mia moja na tano, hizi nyumba mbili za bunge, National Council na National Assembly ni gani. Na kwa lugha ingine National Council unaweza kuiita Upper House na National Assembly ukaita Lower House. Na tunaambiwa kwamba watu watakaoingia National Council watakuwa ni watu kuanzia sabini watakaochaguliwa kutoka kila constituency. Halafu kutakuwa na viti vingine thelathini ambazo zitawekwa kado na watu ambao watachaguliwa ni wanawake kulingana na provinces. Na tunaambiwa kwamba katika hicho kifungu, constituencies zinaangaliwa ni kama districts. Kwa hivyo tukisema kwamba watu sabini watatoka kutoka constituency tunamanisha kila district itachagua mtu mmoja kuenda katika National Council.

Halafu kwa upande wa akina mama kwa sababu ya affirmative action watatoka katika kila province, na kila province tutaelezewa baadaye zinatoa akina wamama wanne. Kifungu cha tatu kina sema katika 1/3 ya watu thelathini kila province itatoa akina mama wanne, lakini Nairobi sio Province ambayo ni capital itatoa akina wamama wawili. Mmeelewa hivyo? Lakini kama hamkuelewa nitafafanua zaidi.

Halafu kifungu mia moja na saba, kina tueleza akina nani wataingia katika National Assembly na tunaambiwa hapo tutafanya election ambayo inafanywa kupitia kitu kinachoitwa Mixed Member Proportional System (MMPS). Na watu ishirini na moja watachaguliwa kupitia system hiyo, na kuna watu wengine tisini ambao watachaguliwa kulingana na list zitakazotolewa na political parties. Watu ambao watachaguliwa kwa MMPS watachaguliwa kawaida na atakaepata kura zaidi ndiye atakaekuwa mshindi; na hii ingine tunaambiwa ya watu tisini vitagawanyishwa kulingana na chama ambacho kitakuwa na viti vingi zaidi. Mumeelewa? Na hapo sasa vyama vimeambiwa katika hiyo 90, list yao lazima waonyeshe ni akina nani mambo kama hayo yanatendeka South Africa hata sio mambo hayatendeki nchi zingine. Sasa kila chama kitatoa list ya watu na wataambiwa kulingana na watu wale wataingia Bunge sasa wataambiwa party A, you will give us 20 kwa sababu muko na watu kadhaa wa bunge, wata rank kulingana na watu wale wameingia bunge. Unaambiwa party A unatoa kumi party B, tano hivyo hivyo. Na hizo party zinaambiwa katika hizo list wanaweka ranking wanasema kama Mr. Willy tunataka mkitupatia ranking mtupatia ranking one ama kama ni councillor munaweka number 2. Kwa hivyo kulingana na viti vile mnapewa mnapatia hao watu kwa priority. Mumeelewa? Na hiyo priority sheria inasema ikiwa number one ni mwanamume number 2 akuwe ni mama. Ikiwa number two ni mama number one awe ni mwanaume. Mumeelewa? Sio wote wanaletwa huko wawe ni mama ama wote wanaletwa huko wakiwa ni baba. Tumeelewana? Na pia katika hiyo list ni lazima vyama vizingatiwe watu walemavu, vijana na vikundi ambavyo ni vya watu wachache, na ni lazima majina yao yawe na national character. Sio kama ni DP majina yao iwe ni

Wakikuyu tu, hapana. Iwe National character, watu watoke sehemu zote za nchi. Hiyo ni mfano tu.

Halafu tumepewa qualifications, ni watu gani ambao wataweza kuwa wanachama wa Bunge. Tunaambiwa ni lazima awe ni Mkenya, ukitaka kuingia katika Upper House ama National Council ile ya kutoka kwa district, ni lazima uwe na miaka thelathini na tano kuendelea juu. Ikiwa unataka kuingia Lower House ile ya kupigiwa kura katika constituency ile ya kawaida uwe na miaka ishirini na moja na pia uwe ni mtu ambaye unaweza kupiga kura. Na ni lazima uwe na elimu ya kidato cha nne, uwe ni mtu ambaye anaweze kuzungumza Kiswahili na Kiingereza; na watu walemaru wawe ni watu ambao wanaweza kuzungumza na sign language ama kusoma braille.

Na pia tumetoa utaratibu ambao utazingatia tabia za watu ambao wanaenda kwa bunge na ni lazima uweze kupita huo mtihani kulingana na hayo masharti. Na je ni nani ambaye hawezi kuingia katika bunge? Ni mtu ambaye hana akili sawa sawa, mtu ambaye ni bankrupt, mtu ambaye amechaguliwa katika ofisi ya kiserikali, mtu ambaye ako jela, na mtu ambaye aliweza kufungwa jela miaka kumi kabla ya kutaka kupigania hicho kiti, na mtu ambaye ametolewa katika ofisi ya umma kwa njia ambayo kwa sababu ya tabia ambayo haikufaa.

Kifungu cha 109 kuhusu akina mama katika bunge tunaambiwa kwamba, kila nyumba hizo mbili ni lazima ziwe na 1/3 ama asilimia tatu ya akina mama, asilimia thelathini ya akina mama. Akina mama wamefurahi mimi nafkiria. Halafu tukapewa jinsi ambavyo watu wa bunge watachaguliwa na pengine kitu ambacho mngependa tuangalie ni kifungu mia moja na kumi na mbili, kuhusu jinsi ambavyo wabunge wanaweza kurudishwa nyumbani, na tunaambiwa wapigaji kura wana haki ya kurudisha MPs nyumbani lakini kupitia utaratibu ufuatao. Ikiwa MP amekuwa mgonjwa hajiwezi kimwili, na akili zake hazifanyi kazi, ikiwa amekuwa na tabia mbovu ambazo zinachochea fitina na kuleta vita katika jamii, na mtu ambaye anakosa kuja constituency kujishugulisha na kuzungumza na watu wake na hana sababu sawa sawa. Na ikiwa mambo hayo matatu yametokea, ni lazima wapiga kura wafanye petition, wapendekeze kwa Speaker, na wapate kura ya asilimia thelathini ya wapiga kura ambao wamejiandikisha katika hiyo constituency, 30% of registered voters.

Naye Speaker akipata habari hiyo ataandikia Electoral Commission na kuwaambia wafanye upetelezi na kuona kama mambo hayo, ni ya ukweli kwa vile inaweza kuwa ni propaganda. Na akipata kwamba repoti imehakikisha maneno hayo speaker atawenza kutangaza kwamba kiti cha hicho constituency kiko wazi, na kueleza kisababu na baadaye sasa kutaweze kuchaguliwa kiongozi mwengine.

Kifungu mia moja na tatu kinatueleza kuhusu Speaker na Deputy Speaker wa National Council watakavyo chaguliwa, 116 inatueleza speaker na Deputy Speaker wa National Assembly hizo mnawenza kusoma. Na pia tunaeleza vile clerks wanaweza kupata kuchaguliwa – wa National Assembly. Halafu kifungu mia moja ishirini kinasemekana kwamba vyama ambavyo havikuunda serikali vitatakuwa kuchague kiongozi wake, leader of minority party kwa sababu majority party imeunda party. Chama kitakachochaguliwa na watu wengi kimeunda serikali hata vyama ambavyo havina watu wengi litatakiwa kuchaguliwa

mkubwa wao ambaye ataweza kuwa na kazi ifuatayo inasemekana katika shuguri za kitaifa atapewa nafasi baada ya Prime Minister na atashughulika na kuenda katika shughuli zote za kitaifa za kuzungumza kwa parliament kwa sababu Prime Minister ndiye atasimamia shughuli za serikali huyu ataweza kujibu maneno yatakayosemwa na Prime Minister, sasa hii inatolewa official sio ati Speaker atampatia nafasi kulingana na katiba ataweza kuzungumza na kujibu mambo yatakayosemwa na Prime Minister na kutuelezea zaidi.

Mishahara ya wabunge, kwamba mishahara ya wabunge kulingana na hii katiba mpya na marupu rupu yatakuwa yana angaliwa na tume maalum na sio bunge; na kwamba mbunge asifanye kazi ingine yejote ambayo ni ya kifaida ama kujihusisha na shughuli yejote ambayo itamkosesha kufanya kazi yake kwa njia iliyo bora. Halafu tunaelezwa shughuli za Parliament na tumeelezwa tukaambiwa kwamba wataweza kupitisha miswada katika Parliament ama Bills, na wataweza kurekebisha sheria za nchi. Watatazama consolidated funds, ama pesa ambazo ni za serikali ama za umma, wataweza kuhakikisha kwamba pesa hizo zimetumiwa kwa njia iliyo bora. Wao ndiyo watajishugulisha na kuweza kupata mikopo na sisi tutalipa na shuguli zote ambazo ni muhimu kwa kazi yao. Sasa haya maneno ya Parliament mtasoma muelewe ili tuweze kuangalia chapter zingine.

Ningetaka tuangalie chapter ya nane kuhusu the Executive, na tunaambiwa kwamba serikali kuu itafanya kazi yake ya kuweka maanani, umuhimu wa watu wa kawaida na kwamba mtu atakaikuwa kiongozi atapewa nguvu ya kuweza kutumikia wananchi, sio kutawala na kwamba kazi yake ataitekeleza kulingana na katiba ya nchi na tukaelezwa shughuli za President katika kifungu mia moja hamsini. Mkisoma mnaona tuaambiwa kwamba atakuwa Head of State atasimamia Jamhuri, atakuwa Commander in Chief atasimamia kamati ya usalama wa nchi na atakuwa ni Mwenye Kiti wa Defense Council. Inasemekana yeje ndiye anasimamia umoja wa nchi, na aweze kuweka watu wote pamoja na kuhakikisha kwamba haki za kimsingi na haki za kibinadamu zinatekelezwa na aweze kuchunga na kukuza katiba ya nchi. Hiyo ndiyo kazi ya President. Na kwamba kama tulivyo sikia hapo mbeleni President hawezi kuwa na cheo katika chama cha kisiasa.

Halafu tunaelezwa pia atakuwa anafanya nini kingine. Hapo mbeleni nimewaambia uwezo wake. Sasa ataweza kujishughulisha na kazi gani. Kazi yake ni kufungua na kuhutubia Parliament – atafungua na kuhutubia Parliament mara moja kwa mwaka. Anaweza akipenda kuhutubia Parliament ama kuzungumza na Parliament na akaweza kuvunja parliament kulingana na kifungu 142. Pengine tuangalie hiyo 142 imesema aje ili tujue vile atavunja Parliament.

Tunaambiwa kwamba National Council itakuwa inafanya kazi kwa miaka minne, Lower House itafanya kazi kwa miaka mitano, na kwamba Parliament haiwezi kujiongezea muda wake ila kupitia kura ya asilimia sitini na tano ya Parliament. Na kwamba hata wakijoingezea isipite miezi kumi na miwili. Na kwamba ikifika tarehe thelathini November wa mwaka wa nne, na wa mwaka wa tano wa hizo nyumba, zitakuwa zime funjwa. Kwa hivyo tunaambiwa Rais hawezi kuvunja kinyume cha hiyo sheria, lazima afuate sheria na hizo tarehe zimewekwa hapo ndiyo aweze kuvunja bunge. (interjection)

Speaker: Kuna sababu zingine za 143 za referendum.

Com. Abida Ali Aroni: Now I am looking at specific provisions. 151 is discussing dissolution by the President. The other one is no confidence of the Prime Minister by parliament. Sasa hizo ni tofauti mimi naangalia kuhusu Rais. Asante.

Tunaelezwa kwamba pia Rais ataweza kuteua na kufuta kazi watu wafuatao, cabinet ambayo itakuwa na Prime Minister ambaye atakuwa ni kiongozi wa chama ambacho kina watu wengi katika Bunge, ataweza kuteua na kufuta manaibu wa Prime Minister, na pia kuteua na kufuta ministers ambao wasio zidi kumi na watano ambao watakuwa wamechaguliwa na Prime Minister. Prime Minister anachagua lakini Rais ana appoint. Mnaelewa?

Na pia Deputy Ministers ambao watachaguliwa na Prime Minister, lakini watakuwa appointed na President; na pia ma officer wa korti na ofisi yejote kama inavyotakikana na hii katiba. Na pia inasemekana kwamba Rais anaweza kujadiliana na cabinet na baada ya kujadiliana na wao akaweza kuteua tume na pia akaweze ku-sign mkataba wowote ambao ni mkataba na nchi zingine za kigeni. Na pia baada ya kuzungumza na kujadiliana na Bunge na Tume ya kulinda salama anaweza kutambua kwamba Kenya iko katika hali ya hatari ama tunaenda kwa vita. Na pia Rais anaweza kuteua watu ambao wako katika hiki kifungu kama ma- Ambassadors ambao wanaenda kutuwakilisha huko nje; na pia Rais anaweza kuomba Supreme Court kumsaidia na kuweza kutoa interpretation ama ikiwa kuna kifungu cha Katiba ambacho hakieleweki inaomba korti inafafanua. Na pia anaweza kusamehea watu ambao wamefungwa. Na pia tunaelezewa kazi ya Rais katika Bunge. Tunaambiwa katika Bunge anaweza kuanzisha ama kupendekeza sheria na anaweza kujadiliana na Cabinet ikiwa anataka kuwe na mswaada ambao utapitia kwa serikali au anaweza kupitisha huo mswaada kupitia kamati yeyote ya Parliament.

Na ikiwa kuna mjadala umejadiliwa na kupitishwa na Bunge, Rais anaweza kufanya mambo yafuatayo. Anaweza kukataa ku-sign na akarudisha Parliament kwa sababu anataka mambo fulani yafanywe, anaweza kuomba hiyo korti ya Supreme Court impatie maoni kuhusu jambo hilo au anaweza ku-sign na kuirudisha Parliament ikiwa amependezwa.

Halafu kifungu mia moja ishirini na nne tunaelezwa jinsi nguvu ya Rais inapunguzwa. Inasema kwamba ikiwa Rais hayuko mtu yeyote ambaye atashikilia mamlaka ya Rais atafanya vipi. Na inatuambia mtu huyo ambaye si Rais lakini anashikilia mamlaka ya Rais hataweza kufanya mambo yafuatayo. Hataweza kuteua wafanyi kazi wa mahakama hataweza kuteua tribunal itakayo zungumza, ama kutaka kuondoa mfanyi kazi wa mahakama na hataweza kuteua mtu yeyote katika ofisi, public office, na hataweza kutoa mtu yeyote ambaye ana-represent mtu Kenya katika Embassy yoyote, na hataweza kumpatia mtu yeyote heshima ya kitaifa. Na mifano nii ni kama Rais ameondoka kuenda safari na makamu wake akashikilia kiti, au ikawa pengine ni mgonjwa na hayuko pengine katika ofisi ameenda leave, na mtu akapatiwa mamlaka ya siku kidogo asiweze kufanya mambo hayo.

Article 155 inatueleza siku ambayo tutakuwa na uchaguzi wa Rais na tumelezwa mtu atakayeweza kuwa Rais ni mtu wa aina gani. Tumeambiwa ni awe mwanakenya, awe na zaidi ya miaka thelathini na mitano lakini isizidi miaka sabini, awe ni mtu ana

tabia safi, awe ni mtu ambaye amesoma na kupata shahada ya degree, awe ameteuliwa na chama cha kisiasa, na ikiwa hana chama cha kisiasa awe ameteuliwa na watu elfu moja kila province apate sahihi ya watu mia moja. Sasa maneno ya rais yamezungumzwa sana mpaka kifungu 164, lakini ningetaka tuangalie kifungu 155 kuhusu ofisi ya makamu wa Rais. Na tunaambiwa kwamba kila mgombeaji wa kiti cha Rais achague mtu atakayesimama na yeze na huyu Rais akishida huyo mwenzake atapata kiti cha Vice President. Anaitwa running mate kwa Kiingereza, na kwamba hakutakuwa na kura tofauti na President atachaguliwa pamoja na mwenzake ambaye ni President. Na kwamba ofisi na wakati wa vice President utakuwa ni wakati ambapo Rais anaanza kazi na wakati ambapo kazi ya huyu Rais imeisha. Na tukaelezewa kifungu 167 kazi ya makamu wa Rais tunaambiwa yeze atakuwa ni msaidizi wa Rais katika kazi zake na kwamba atafanya kazi zingine zozote atakazopewa na Katiba; lakini Rais anaweza kumpatia kazi ya kufanya mara kwa mara na kwamba makamu wa Rais hataweza kuwa na ofisi nyininge yejote ya kiserikali, na katika chama cha kisiasa ama pahali pengine popote analipwa. Na kwamba Rais akiwa hayuko na akiwa ni mgonjwa atakayesimamia mamlaka ya Rais ni Vice President.

Tumeelezwa kuhusu mishahara yao itaangaliwa na ile ile tume kama mishahara ya MPs. Halafu tunapewa kazi na shuguli za Prime Minister na tunaambiwa kwamba Prime Minister ndiye atakuwa mkuu wa Cabinet na atashugulikia sehemu zote za serikali. Prime Minister ateweza kutengeza na kutekeleza budget ya nchi. Kazi yake pia itakua kuanzisha miswaada na sheria katika Bunge. Itakuwa ni kazi yake kuhakikisha kwamba sheria zote zinatekelezwa ambazo zimetungwa na Parliament. Yeye ndiye atasimamia na kuhakikisha kwamba shuguli zote za ministries na departments zimetekelawa na atafanya kazi yejote ambayo atafanya kutekelezwa na bunge kuhusiana na shuguli za kiserikali.

Nani atakayemchagua huyu Prime Minister? Tunaambiwa Lower House ndiyo itachagua Prime Minister na President atapendekeza kwa Speaker jina la mtu ambaye angependa awe Prime Minister. Na mtu huyo ambaye angependekezwa anatakiwa awe ametoka katika chama kilicho na watu wengi katika Bunge, au mkusanyiko wa vyama; coalition ya vyama ambazo ziko katika Bunge. Na ikiwa huyu leader ama msimamizi wa chama kilicho na watu wengi bungeni hana uwezo wa command ama mambo yake hayapendezi watu ambao wako katika National Assembly, Lower House yule ambaye atakuwa ni leader wa minority party atapewa nafasi ya kupendekeza jina. Ikiwa watu hawa wawili hawakuweza, mtu mwingine yejote katika chama ama MPs anaweza kupendekezwa na President kama Prime Minister. Na wakati ambapo President atapendekeza kwa Prime Minister, Prime Minister ataita bunge na kupendekeza hiyo jina baada ya kupata hiyo jina kuitia siku saba na hapo Prime Minister atachaguliwa na njia hizo tatu.

Prime Minister atafanya kazi yake hadi wakati ambapo atastaifu, ama atakufa au mpaka atakapotolewa ofisi na Rais kuitia Bunge, na pia wakati ambapo tutakuwa tumekwenda kura zifuatazo. Prime Minister inasemekana anaweza kufutwa kazi kuitia bunge asilimia hamsini ya watu ambao ni members watasema kwamba wamekosa imani na huyo Prime Minister na hapo President itabidi kumfuta kazi. Halafu tumeelezwa kuhusu Cabinet nafikiria hapa hakuna mambo mengi isipokuwa kwamba Ministers na Deputy Ministers wasichaguliwe kutoka Bunge wachaguliwe kutoka nje ya Bunge. Na tukaelezwa vile watakavyo fanya kazi na jinsi watakavyokuwa wanahudumia wananchi. Chapter tisa wanaongea kuhusu mahakama na tunaambiwa

kwamba nguvu zetu kama wananchi wa Kenya katika hii sehemu ya sheria imepewa korti kupitia wananchi. Na kwamba mahakama yatahakikisha ya kwamba sheria zinafuatwa na kwamba uhaki au kesi hazicheleweshi kortini, na kwamba bila tu kufanya kesi mahakama itajaribu kuunganisha watu kupitia njia zingine za kuwalete pamoja kabla hazijafanya kesi na kwamba mahakama itazingatia mambo ya kikatiba. **End of tape 2A.....**

Na kwamba korti ya juu zaidi iwe Supreme Court halafu ifuatwe na korti ya rufani ambayo ni Court of Appeal, halafu ukitoka kwa Court of Appeal unakuja High Court na baadaye tunakuja kwa Magistrate Court.

Na katika Magistrate Court tutakuwa na korti ya Waislamu inayoitwa Kadhi's Court na korti yoyote ambayo pengine itawekwa na Bunge na pia korti za kienyeji, traditional or local tribunal kulingana na vile Parliament itakavyotoa sheria. Na kazi ya Supreme Court ni gani? Tunaambiwa Supreme Court itaweza kufanya kazi ifuatayo: kutoa maoni kwa President wakati ambapo atawauliza ikiwa kuwa kuna petition ya kura ya President itafanyiwa huko kwa Supreme Court, na pia wakati ambapo tutataka kufanya impeachment – kutoa President kwa sababu amekosea katiba ama amekosea wananchi na tunataka aondolewe, hiyo kesi inaweza kupendekezwa kwa Supreme Court. Ikiwa kuna mtu yejote anapinga sheria itakayoteuliwa na Parliament na kusema kwamba sheria hiyo haiambatani na Katiba utaweza kuenda katika Supreme Court, na pia ikiwa kuna matatizo baina ya District Council ya utawala na National Government, mambo hayo yatapendekezwa katika Supreme Court.

Court of Appeal tunaambiwa itafanya kazi gani, nafikiri itafanya kazi ile tu inafanya wakati huu kusikiza rufani ama appeals zitakazotoka kutoka High Court, ama katika korti nyingine yejote kulingana na sheria. High court itafanya kazi yake kama kawaida tutasikiza criminal na civil court cases.

Magistrate's Court itaendelea kufanya kazi yake kama kawaida halafu tuangalie kifungu 168 jinsi ambavyo majudge watakanan na ofisi na tunaambiwa kwamba maofisa wa korti wote hata majudge watastaifu wakiwa na miaka 65. Kwa wakati huu wanastaifu wakiwa na miaka 74 lakini akifika 60 akitaka kustaifu akubalishwe.

Na tunaelezwa jinsi watakavyo ondoleshwa kwa kazi. Tunaambiwa Judge ataondolewa kwa kazi yake ikiwa amekuwa mgonjwa na hawezi kutekeleza kazi yake kwa sababu ya maradhi hayo, ikiwa amekosa kuweka nidhamu, ikiwa amekosa kufanya kazi yake kwa njia inayostahili. Na tunaambiwa kwamba ikiwa kuna mtu binafsi, kuna kikundi cha watu ambao wangetaka Judge kuondolewa watafanya mapendekezo kwa Judicial Service Commission. Hii ni Tume itakayowekwa haiko kwa wakati huu lakini imewekwa nguvu zaidi ya kutekeleza shughuli za kortini. Na ikiwa mtu atafanya mapendekezo yakumuondo Judge, basi Judicial Service Commission yakipata mapendekezo hayo watamuomba Rais kutengeza tribunal ili isikize kesi isije ikawa Judge huyo ameonewa ili akiondolewa ofisi aondolewa kwa njia iliyo ya haki na iliyo sawa.

Article 204 pengine mungetaka kuangalia Judicial Service Commission – watu ambao watakuwa kwa Judicial Service Commission ni watu gani. Tumeambiwa kutakuwa na fulltime chairman ambaye ni mtu anaweza kuwa ni Judge wa mahakama, wataweka mwanamke wa Kiislamu, wataweka Attorney General, wataweka Judge moja kutoka kwa Supreme Court, Judge

moja kutoka kwa Court of Appeal, moja wa High Court, kutakuwa na Chief Kadhi, kutakuwa na Mahakimu wawili na mmoja lazima awe ni Magistrate awe ni mwanamke, mawakili wawili mmoja awe ni mwanamke, waalimu wawili wa sheria na mmoja lazima awe ni mwanamke, na kutoke na mtu kutoka kwa kamati ya mafunzo ya sheria, atoke Chairman wa Public Service Commission, na watu watatu ambao ni wananchi wa kawaida, na katika hao watu watatu lazima mmoja awe ni mama na watachaguliwa na chama kikuu cha vyama visivyo vya serikali, na watu hawa watafanya kazi yao kwa muda wa miaka mitano na zaidi ni miaka kumi. Hawawezi kupitisha siku hizo. 205 tumetoa functions zao watakazofanya tumeambiwa wata-recommend kwa Government ni nani atakayechaguliwa kama Judge, nani atakaechaguliwa kama Magistrate, ama kufanya kazi kwa mahakama. Wataweza kuangalia jinsi magistrate wanafanya kazi kuwapatia discipline, watajaribu kuzidi kuwasomesha mahakimu na majudge ili waweze kufanya kazi yao sawa sawa. Wataweza kueleza serikali jinsi ambavyo sheria inaendelea katika nchi, watajaribu kuhakikisha kuna usawa wa haki katika utekelezaji wa kazi za kisheria, na watafanya kazi ingine yejote watakayopewa na bunge.

Mkuu wa sheria kifungu 208, kwamba kutakuwa na mkuu wa sheria ambaye atateuliwa na Judicial Service Commission; halafu jina lake lipendekezwe kwa President ambaye hawezi kuteua ikiwa Upper House haijakubali na kwamba mtu atakayeteuliwa kama mkuu wa sheria awe ni mtu ambaye anaweza kuwa ni Judge wa mahakama kuu, na yeje ndiye atakayekuwa ni msamimizi wa sheria katika serikali na ni kazi yeke kuu kuhakikisha kwamba tuna utawala wa kisheria katika nchi.

Halafu kutakuwa na mtu anayeitwa Director of Public Prosecution. Kwa hivyo ofisi ya Attorney General kwa wakati huu itagawanishwa mara mbili. Mmelewa? Na mtu hata ambaye ako saa hii anaitwa DPP atajisimamia, hatakuwa chini ya mkuu wa sheria, na kazi yake itakuwa kusimamia kesi zote za serikali na atateuliwa kupitia kwa Public Service Commission na approval ya Upper House. Na pia aweze kuwa ni mtu anaweza kuwa Judge Mkuu wa mahakama kuu ya Kenya, na anatakiwa kufanya investigation ya kesi zote ambazo ni kesi za criminal nature, kesi ambazo sio za kibinaffsi, na inasemekana hataweza kuondoa kesi kwa wakati huu. Hata mapolisi wale mnaona wako katika chini ya Director of Prosecution hawataweza kuondoa kesi yejote kwa korti bila kuomba ruhusa ya korti. Kwa sababu wakati huu wanakuja wanaondoa wanasema tu we wish to withdraw. Sasa korti haina ya kusema. Sasa wanaambiwa ni lazima waeleze korti kisababu na korti ikubali. Na kwamba ikiwa anataka kuanzisha kesi yejote hatakiwi kuomba ruhusa ya mtu yejote anaenda straight kwa korti na kuanza hiyo.

Halafu tutakuwa na public defender ama Ombudsman- 210- Huyu atachaguliwa na Judicial Service Commission kupitia kwa Upper House; halafu ateuliwe na President. Na kazi yake ni kusaidia wananchi wa kawaida ambao watakuwa hawawezi kuwa na pesa za kuweka mawakili. Ataeleza wananchi wa kawaida maneno kuhusu sheria; na pia bunge itaweza kutengeza sheria itakayo muwezesha mtu huyu kufanya kazi yake sawa sawa bila pingamizi yejote.

Halafu kuna 212 kuhusu mawakili, legal profession, inasemekana kwamba watu ambao wanafanya kazi ya mawakili wanatakitana kuhifahadhi nidhamu ya hali ya juu, kwa sababu ni watu kawaida wamepewa heshima na kuaminika na wananchi

wa kawaida. Ni lazima wazingatie na kuhifadhi katiba ya nchi, waweze kuhifadhi haki za kibinadamu, waweze kufanya kazi yao kwa njia iliyo bora bila kusumbua wateja wao. Na kwamba wakiwa katika korti watafanya kazi yao bila kuogopa wakizingatia interest ya customer wao, wataweza kusaidia mahakama kukuza sheria na kueleza korti sheria ambazo zinaweza kufaa; kazi yejote bila kumdhuru customer wake.

Chapter 10 devolution of power. Katika devolution of power 213 tunaangalia ni mambo gani ambayo inazingatiwa katika devolution, au katika kuleta utawala karibu na wananchi wa kawaida. Tunasema kwamba kwanza kabisa ni kuleta utawala karibu sana na wananchi ili waweze kujihusisha kupitia kwa jamii zao tofauti, na pia kufanya hivyo tuone kama tutapata kukuza umoja wa wananchi. Pia kuweza kuweka demokrasia na uwazi katika utawala. Kuweza kuwa na checks na balances. Kuona kwamba kuna nidhamu na kila mkono wa serikali unafanya kazi yake bila kuingiliwa na chombo hicho chingine. Na pia kuweza kukuza uchumi. Kuona kwamba tumegawanyisha rasilimali ya Kenya kwa njia inayofaa mbila mapendeleo, na ikiwa kuna sehemu ambazo ziko nyuma zikaweze kuangaliwa zaidi kujaribu kuzikuza zitoshane na sehemu zingine. Kujaribu pia kuondoa serikali kutoka kwa central government, serikali kuu na kuleta serikali karibu na wananchi.

Kuweza pia kuwapatia huduma wananchi kwa njia iliyo sawa, iliyo rahisi kwa kifedha pia kuweza kuangalia masilahi na kukuza masilahi ya watu ambaa wametengwa, marginalised, or minority or the disadvantaged groups. Na pia kujaribu kuwa na uhusiano wa vyombo tutakavyotumia katika kusambaza utawala. Na inasemekana kwamba hivyo vyombo vitakavyotumika katika kusambaza utawala zinatafaa kuhudumiwa kifedha sawa sawa. Na pia kupata pesa kutokana na rasilimali ambazo ziko karibu na wao, na tunaangalia ni nini tutafuata tukatekeleza hayo mambo. Ni kwamba vyombo ambavyo tutakavyotumia na tutavyona katika kifungu 215. Ni lazima viwe vimewekwa kutumia msingi ya kidemokrasia ili watu wale watakaa katika vyombo hivyo wale wamechaguliwa na kuwekwa pale kuzingatia demokrasia, na kulingana na katiba hii wakitengeza sheria yejote au utaratibu wowote, ni lazima wafuate mambo ambayo yako hapa; na wakuu wa vyombo hivyo ni lazima wafanye kazi yao kwa uwazi, na waweze kuwa accountable kwa wananchi wa kawaida. Na kwamba wananchi wakiwa wamechagua wakubwa hao waweze kuwarudisha kama tunavyosema ma MPs wanavyorudishwa, na kwamba katika vyombo hivyo lazima watakao kaa kule asilimia thelathini wawe ni akina mama.

Na je vyombo hivyo vitakuwa katika kiwango gani? Tumeviita village government ama sublocation government, tutakuwa na utawala kwa vijiji. Tukisema government labda mnaweweza kushidwa tutakuwa na Rais ama ni nini? Hapana ni watawala katika level ya kijiji. Kwa sababu tulipokuwa tunaenda kuchukua maoni tuliambiwa kuna wazee wa vijiji wanafanya kazi lakini hawatabulikani, sasa tukasema utawala uanze katika vijiji na tunesema kwamba hiyo village council ama village government; iwe ina wazee wa vijiji au kama kuna kijiji chochote kinaona si sawa wanaweza kufanya kura ya kuchagua watu watakaokaa katika hiyo village council, na watu hao wasizidi kumi na wasipungue sita. Na pia wao wenyewe watatengeza jinsi wangetaka kufanya kazi katika kijiji chao kwa sababu ukitaka kuanshiza mambo mengi kwa kijiji pengine watu tofauti wana mila tofauti zinaweza kosa kusikizana.

Tukitoka katika village kwa sababu hiyo ndiyo ya chini kabisa tunaenda location, na tunaita location council; nayo hiyo itakuwa na wakiilishi wawili kutoka katika kila village ya hiyo location. Na katika hao watu wawili lazima mmoja awe mama, sio wanaume wawili ama wamama wawili. Mwanaume mmoja..lakini vile sheria inasema hata mkipeleka wamama wawili ni sawa – one of whom shall be a woman. Haijasema lazima awe mwanaume. Na lazima wachaguliwe na hiyo kamati ya wazee. Hiyo kamati ya wazee ndiyo itatuma representative wawili katika location. Na hapa ndiyo administration yote itakayofanywa hata ya village council. Halafu tukitoka village council ingine inakuwa ni district na katika vyombo hivi vinne kwa sababu tukitoka kwa district tunaenda kwa province itakayokuwa na nguvu zaidi ni district na sio province. Na district ndiyo wataweza kutengeza sheria zote ambazo zitatengezwa na district council na district council itakuwa na watu wasipungue ishirini na wasizidi thelathini. Between twenty and thirty - Members of the District Council; na hawa watachaguliwa by vote. Mtu yule anataka kuwa kwa District Council anaenda kupigiwa kura Na watachaguliwa na watu ambao wamejiandikisha kwa kura na wataweza kuwa na watu ambao watafanya kazi kwa district watateuliwa na district council sio serikali kuu. Na ikiwa kwa mfano wanataka kuwfuta itawabidi wapige kura ya members ili kufuta kama Chief Officer ambaye atakuwa anasimamia shuguli zao.

Halafu tukitoka hapo tunaenda kwa Provincial Government ama Provincial Council na tunaambiwa kwamba watu watakaoenda kwa Provincial Council watakuwa representative wawili kutoka kila district na lazima mmoja awe mama. Na ukiangalia 220 inatupatia nguvu za district council na unaona tunaambiwa district council ndiyo itakuwa sehemu muhimu ya utawala – principle level of devolution of power. Mambo yote yatafanyika ya kitawala katika district. Na ukiangalia seventh schedule itakueleza zaidi kuhusu kazi ya district government. Halafu tumepewa kazi itakayofanywa na provincial government, tumeambiwa kazi yao ni kukuza uwezo wa council ya district na kuweza kuweka cooperation katika district hii, na province na pia kusaidia district kufanya kazi yake na kuweza kuwatengezea utaratibu wa kutumia fedha za district, na pia kuweza kusimamia institutions ambazo ziko katika province. Hiyo ndiyo kazi ya provincial government. Kwa hivyo mambo yote kama nilivyo sema iko katika district.

Halafu kwa upande wa Nairobi – Nairobi itakuwa na kitu kinaitwa urban government. Kwa sababu inasemekana Nairobi iko na msimamo wa kibinasi ikiwa ndiyo capital city Na maneno yake sheria itatungwa na Parliament na kusema vile Nairobi itajisimamia. Zingine nafikiri mtasoma muone vile devolution itakavyo fanya.

Chapter 11 inazungumza kuhusu shamba na mali. Tunaambiwa kwamba kila mwananchi atapata nafasi ya shamba na kwamba walionunua mashamba na kumiliki mashamba na njia iliyo bora watahifadhiwa na kuchungwa na serikali. Tunaambiwa pia jinsi ya kuchunga na kuhifadhi mazingira. Tunaelezwa kwamba pia mashamba yote au ardhi yote ya nchi hii ni mali ya wananchi wa Kenya; either akiwa ni mtu binafsi ama kupitia kwa jamii, na kwamba mtu asiyehi mwananchi wa Kenya hawezikuwa anamiliki ardhi nichini Kenya, na kwamba mwananchi wa Kenya anaweza kumiliki ardhi sehemu yeoyote ya Kenya.

Kifungu 234 tunaelezwa kuhusu shamba ambazo ni za umma. Halafu kifungu 236 tunaelezwa jinsi ambavyo serikali itaweza kuchunga ardhi, na pia tunaambiwa kwamba serikali isichukue ardhi ya mtu bila kisababu cha kutosha. Lakini ikiwa ina

kisababu inaweza kuchukua ardhi na kuweza kulipa mtu huyo, na pia tunaambiwa kwamba kutawekwa Tume ya kusimamia mashamba ambayo ni ya umma.

Chapter 12 inazungumzia mazingara na mali ya asili. Tunaambiwa kwamba ni jukumu letu kama wananchi wa Kenya kuweza kusimamia na kuhifadhi mazingara na mali ya asili ya nchi hii. Na kwamba serikali ina jukumu ya kuuliza wananchi kujishugulisha na mambo ambayo ni ya manufaa katika mazingara ya nchi. Na kwamba serikali itambue na kukuza njia za kitamaduni na kusimamia mali ya asili na mazingara. Na pia ikiwa tamaduni hizo sio tamaduni ambazo zitakwenda kinyume na katiba na haki za kibinadamu. Tunaelezwa pia serikali ni lazima katika kazi yake kuhakikisha kwamba ina fanya kazi hiyo na kupitia mambo ifuatayo: kuchunga wanyama wa msituni na mali zingine, kuchunga misitu na kuweza kuomba na kusihwanananchi kuchunga hiyo forest na pia tunaambiwa ni lazima serikali iweze kuchunga sehemu za maji na pia kuhimiza wananchi kufanya hivyo na pia jinsi ambavyo serikali itachunga environment na kuhakikisha kwamba hakuna uharibifu; na kwamba serikali itakuwa wazi, na kukubalisha mwananchi wa kawaida kuzungumza kuhusu mali ya asili na mazingara. Na kwamba kutakuwa na kama Tume hivi ambayo itazingatia mambo kama haya na tumesema itateuliwa tume inayoitwa National Environmental Management Committee, ili ichunge mazingara na mali ya asili ya wananchi wa Kenya. Na kwamba parliament itatunga sheria ambazo zitakuwa zinasaidia utekelezaji wa mambo ambayo yamewekwa katika katiba.

Chapter ya 13 inaongea kuhusu fedha za umma na jinsi ambavyo tunaweza kuchunga pesa hizo. Na tumepewa vipengele ambavyo vinasema jinsi serikali itakavyo angalia mali ya umma. Inasemakana kwamba serikali itafute njia bora itakayotuwezesha kupata hizi fedha ili tuweze kukuza hali ya mwananchi wa kawaida; na pia ni lazima serikali ihushishe wananchi wa kawaida na vyama visivyo vya serikali katika kuchunga mali hii. Na ikiwa serikali inagawa hizi fedha za umma lazima igawe kwa njia ya usawa kote nchini, lakini iangalie na kupatia pengine pesa zaidi sehemu ambazo zimesahaulika na hazina maendeleo. Na kwamba pesa zitakazopatikana zigawanyishwe kwa usawa katika district, province na local government.

Kusiwe na chombo chochote cha serikali kitakacho sahaulika. Na kwamba kabla hajifanya allocation, serikali iweze kuzungumza na watu kutoka sector tofauti ili iweze kugawa pesa sawa sawa. Na kwamba budget na matumizi yake itafanywa kwa njia ya wazi ili kuhakikisha kwamba pesa za serikali zinatumika vizuri.

Halafu kuhusu tax, ama kodi tunayotozwa kama wananchi inasemakana kwamba hakuna kodi itakayotozwa ila kodi ambayo imekubaliwa kupitia bunge, na hakuna mtu yeyote ama sehemu yeyote ya serikali itakayoondoa kodi bila ruhusa ya parliament.

Halafu pia tunaelezwa kuhusu pesa zinazotengwa kuhusu matumizi ya pesa za serikali, na jinsi pesa hizo zitakazotumiwa kupitia bunge. Ni lazima bunge ikubali ni pesa ngapi zitawekwa katika consolidated fund; na zitagawanyishwa vipi? na zitatumika vipi? Mtasoma hizo zingine kuhusu pesa ndiyo tupate wakati wa mazungumzo. Tumeelezwa pia kuhusu Central Bank na deni ya serikali. Tunaambiwa kwamba deni yeyote ya serikali itawekwa katika hii consolidated fund, na kwamba banki kuu ya Kenya ndiyo benki peke yake itakayota pesa za Jamhuri ya Kenya. Tumeelezwa jinsi Governor atakayeteuliwa kupikia kwa Bunge. Tumeelezwa pia kazi ya Central Bank, na ukiangalia pia kazi ya Controller na Auditor General sasa imegawanyishwa. Kuna

mtu anaeitwa Controller General, na kuna mtu anaeitwa Auditor General. Na controller of budget kazi yake itakuwa ni kujihusisha na budget, na tumepewa kazi yake atakayofanya. Inasemekana kwamba lazima ahakikishe ya kwamba hizo pesa zilizotengwa kwa budget zinatumika kama ilivyotangazwa, na ahakikishe kwamba hesabu zote zimebekwa na ziko kamilifu; na kazi yake pia ni afanye kazi na parliament na kuwaelezea, kuwapatia mawaidha na pia kufanya kazi pamoja na ministry ambayo itahusika na kazi ya pesa. Halafu huyu Auditor General pia amepewa kazi yake na kazi yake iko katika kifungu 254, na inasemekana yeze ndiye atakuwa mkaguzi mkuu wa mashirika yote ya kiserikali. Sasa kuna mtu atakayesimimia budget na kuchunga matumizi yake. Kuna yule mtu atakagua matumizi ya serikali, wamegawanyishwa na kuwa watu wawili sasa.

Chapter ya 14 ni kuhusu public service. Public service ni watu wanaofanya kazi kwa mashirika serikali na jinsi watakavyofanya kazi yao na kifungu 258 ukisoma inatueleza jinsi wanafaa kufanya kazi yao. Halafu tumeambwa kuhusu Public Service Commission, ambayo iko kwa wakati huu lakini imepewa majukumu mengine na majukumu yao yako katika 260 watakuwa wanachunguza na kuhakikisha kwamba ma-ofisa wote..... **end of tape 2**.

Tape 3

..... katiba ya wakati huu, vyombo kama vya polisi vya majeshi haziko na hazijahudumiwa na katiba. Kwa hivyo kwa wakati huu tunaelezwa kuhusu Kenya Police Service, itaitwa Kenya Police Service na tumeelezwa kazi yao ni nini. Na tumepewa point kama tisa za kueleza kazi yao ni kazi gani, kueka amani, kuhakikisha na kulinda haki za wananchi, kutupatia security ama usalama, kuhakikisha kwamba hakuna uhalifu na kusaidia watu ambao wamepata madhara kuitia uhalifu na kuchunga mali ya wananchi. Na kwamba mapolisi watajaribu sana kufanya kazi yao kwa nidhamu na hali ya juu wataacha rushwa, watafanya kazi yao bila mapendeleo wa mtu/kikundi chochote cha kisiasa na watajaribu kuzingatia haki za kibinadamu, na watasomesha kwa hali ya juu na kuwa wazi katika kazi yao na kuzingatia demokrasia. Na tunaambwa kwamba kutakuwa na Commissioner of Police ambaye atateuliwa na Rais na atafanya kazi kwa muda usiozidi miaka kumi. Na ni lazima mtu huyo awe amehitimu kwa mambo kadhaa Na tumepewa katika kifungu 266 mtaweza kusoma halafu kifungu 267 tumepewa Kenya Correctional Services hii, ni badhala ya kusema Kenya Prisons, tumebadilisha jina na kuita Kenya Correctional Services na tumeelezwa mambo yao na kisababu ambacho tumebadilisha kutoka Prisons, jela na kuita Correctional Services ni kwa sababu ukiangalia kifungu 267 (1) tunasema umuhimu wa hiki kikosi ni kuweza kuwasaidia na kuwabadilisha wafungwa, rehabilitate. Kuwabadilisha kutoka kuwa watu wabaya ili kuweza kuona kama na kuweza kubadilika na kuweza wakienda nje kuishi maisha ya kawaida wawe ni watu ambao wanaweza kuwa wa manufaa katika jamii. Tukaona ile Kenya Prisons hiyo sio vizuri kwa sababu watu wakienda jela wakitora wanaonekana sio kama watu tena ni kama wanyama lakini pengine ni kwa sababu jera hua haitii mkazo kubadilisha mawazo na tabia ya wafungwa. Na tukasema watafanya kazi yao namna gani.

Halafu chapter ya 15 tunaongea kuhusu the Defense Forces and National Security. Usalama wa nchi na tumeelezwa katika hicho kifungu kazi watakayofanya kuhakikisha kwamba kuna usalama katika nchi na kwamba watajaribu kusomesha members kwa njia ambayo itaweza kuhudumia wananchi kwa njia iliyo bora. Na katika kifungu mia mbili na sabini na mbili (72),

tunasema kwamba tutaweka National Security Council kuwa na kamati itakayosimamia usalama wa nchi, na ukiangalia iko na watu ambao watakuwa ni wanachama wa council hiyo. Kutakuwa na Executive halafu kutakuwa na ma-commander wa Navy, wa Army, wa Airforce, Commissioner of Police, Director of Correctional Services, Director wa Intelligence, na Parliamentary Committee ambayo itasimamia usalama, Attorney General ili ukikumbuka wakati tulisoma ikiwa kutatakikana kutangazwe hali ya hatari, au hali ya vita lazima watu hawa wakae wazungumze halafu ipite katika National Council ndiyo Rais aweze kutangaza.

Sio eti ni kazi ya mtu mmoja. Ukiangalia hawa watu wote watu kumi na watatu, halafu wakizungumza iende kwa National Council sio rahisi kuwe kumefanyika kitu ambacho sio kizuri. Si ni ukweli?

Halafu tumeambiwa kazi yao ya National Council ile watafanya imeandikwa hapa yote. Halafu tumeelezwa pia defense force na tunaambiwa mtu yeoyote huwezi kuanzisha kikosi cha usalama kwa nchi bila kupitia ruhusa ya bunge. Na pia kutakuwa na Defence Forces Council, kutakuwa na National Security Council, lakini kutakuwa pia na Defence Council inayehusika na mambo ya defence. Na tukaambiwa watu wale watakuwa hapo na kazi ile watajishugulisha nayo.

Chapter 16, naona watu wamechoka lakini tutamaliza ndiyo – leadership – mimi nawapeleka juu juu ili muende nyumbani musome. Unajua siwezi maliza hata ni kikaa from 8 to 8. Si ni ukweli? Hii ni kupitia tu kuwapatia morale muende musome. Chapter 16 leadership and integrity. Tunaangalia nidhamu ya kiongozi na tunaambiwa hii chapter itawahusisha watu wafuatao: Rais, Prime Minister, Deputy Prime Minister, Ministers wote, Members of Parliament, wale wote watakaokuwa kwa Local Council kama village, district, provincials and all other public officers; na watu wote ambao watakuwa wameandikwa kazi kupitia kwa katiba kwa sababu umesikia Constitutional Commission. Na tumeambiwa ile responsibility yao, watakuwa na nidhamu ya aina gani? Imeandikwa yote hapa, kwa 277.

Halafu Chapter ya 17 tunaelezwa ni Tume gani itakayowekwa ili kusaidia katika utekelezaji wa kazi ya umma. Na ukiangalia 288 tunaona kuna Human Rights Commission ambayo itatekeleza na kuhakikisha kwamba haki za kimsingi za kibinadamu zinazingatiwa na tumeambiwa kazi yake yote. Halafu tumeambiwa kutakuwa na Ethics na Integrity Commission, na kazi zake tumeelezwa vile itafanya. Tumeambiwa kutakuwa na Salary Remuneration Commission na kumbuka hii itaangalia mishahara ya wakubwa wote, halafu kutakuwa na Teachers Service Commission, itatambulikana na Katiba na kazi zake tumeambiwa itakuwa ni nini. Halafu tutakuwa na Constitutional Commission na tutaambiwa itafanya kazi gani. Na pia tumeambiwa katika 293, kwamba watu ambao wametajwa hapo pia watakuwa wanakaa katika ma-ofisi za kikatiba.

Chapter 18, ni vipi ambavyo katiba itabadilishwa. Tunaambiwa kwamba mtu akitaka kubadilisha Katiba hii yaani Mbunge, atapeleka mswaada kwa bunge na ikipita katika somo la kwanza na la pili, ni lazima iungwe mkono na asilimia sabini na tano 2/3 majority ya wabunge. Kwa wakati huu ni 65 sasa tumeongeza to 75, anyway mtafanya mathematics mimi si mathematician mimi ni lawyer. Kwa hivyo mтанisamehe. Kwa hivyo itakuwa 2/3 majority ya wabunge katika 2nd and 3rd reading na itapelekwa kwa Rais ambaye ni lazima aweke kidole. Na unakumbuka tuliambiwa jinsi Rais anaweza kuweka kidole. Anaweza kuweka kidole bila kusema kitu yeoyote, anaweza kuweka kidole baada ya kuenda kwa Supreme Court, ama

akakataa akarudisha Parliament akasema mfanye hivi na hivi na hivi. Lakini tunaambiwa ukiangalia 294,3 kwamba ikiwa mtu anataka kubadilisha kifungu saba, kifungu ya kwanza ambayo inazungumza kuhusu watu, sovereignty of the people, nguvu ya watu ambayo inataka kutoa kifungu sita ambayo itatoa kufanya haki za kimsingi, ambayo itataka kubadilisha ama kuondoa chapter 10, ambayo itajihusisha na uraia au hii Chapter ya kumi na nane. Ni lazima itumwe kwa wananchi ili kupata kura ya maoni kabla haijaenda kwa Rais. Mmeelewa?

Chapter ya kumi na tisa inaitwa interpretation chapter. Inatueleza maana ya maneno imetumika hapa pengine kawaida ina maneno tofauti. Kama sasa tumeelezwa civil society ni nini, tumeelezwa financial year, political party, subordinate court, vitu kama hizo mnawenza kusoma ili muweze kuelewa maana ya maneno ambayo yametumika.

Chapter 20 tunaelezwa mambo ambayo yata tendeka wakati ambapo tutakuwa tunatekeleza katiba mpya kabla hatujakamilisha kabisa maneno ambayo yanahusishwa na katiba hii mpya - transitional and consequential provision. Halafu tuna first schedule ambayo inazungumza kuhusu mipaka yetu, tuna Kenya, Uganda, tumeelezwa mipaka ya Kenya - Uganda border, Kenya-Sudan, hiyo mtasoma ni maneno mengi, Kenya- Tanzania, Kenya – Somalia halafu schedule ya pili tunaelezwa schedule ya province nane, na Nairobi imetambulika kama province, halafu tumeambiwa district na Nairobi imetambulikana kama district, one district, one province. Halafu tunaambiwa Rift Valley, North Eastern na hizo district ambazo ziko katika kila mkoa. Halafu schedule ya tatu tuna ambiwa symbols, vitu ambavyo vinatambulika kama ni vitu vya kitaifa, bendera, wimbo wa taifa, court of arms, kitu ambacho huwa kinapigwa chapa katika vitu vyote vya serikali halafu tuna seal ambayo ni ya Kenya.

Fouth schedule tunaonyeshwa, viapo vitakavyo somwa kwa kusemwa na Rais na ma executive wote, Permanent Secretary, Prime Minister na watu wote wale watafanya na kuchukua jukumu la kitaifa.

Fifth schedule ndiyo tuna ile leadership na integrity code. Sasa hii mtasoma muone jinsi nidhamu inatakiwa viongozi na kuna mambo mengi mtasoma muone.

Schedule ya sita tunaangalia mapendekezo ambayo yanatakiwa kufanywa na parliament nani kazi gani hiyo na itachukua wakati gani. Kwa mfano, right to access information. Je wananchi watapata aje, kwa muda gani serikali itaweza kuhakikisha kwamba tutaweza kupata maneno yote ambayo yako kwa serikali? Inasemekana miezi sita, kuhudumia ma refugee mwaka mmoja, kuhakikisha sheria zote za Kenya zinaambatana na Katiba mpya tumeambiwa miaka miwili kuhakikisha kwamba sheria zote za mashamba zinaambata na Katiba, miaka miwili and so on and so forth. Mtasoma. Na ni mambo mengi ambayo yatafanya na parliament (interjection) ama hamna? Sixth schedule haiko kwa hiyo gazette? Iko page 45 check page 45 please. Imekuwa colour kidogo labda ndiyo mzee hajaona. Umeona mzee page 45? You are using another one, use ile ya leo hiyo lazima iwe imefanyiwa amendments.

Kuna seventh schedule powers of the National and the District Government; mtaona sasa National government itakuwa na kazi

gani, district council itakuwa na kazi gani; hii mapendekezo msome muone kama ni maneno mzuri.

Halafu 8th schedule inatuambia vile transition provision kabla maneno haya yote hayajatekelezwa na bunge tunaelezwa kuhusu elections. Kwa mfano tunaambiwa section 4 mtu ambaye amekuwa ni Rais kwa zaidi ya term mbili hawezি kusimama kama President, Vice President or Prime Minister pia hawezى kuwa Deputy Prime Minister, Minister or even Member of Parliament. Mtasoma hiyo iko hapo.

Tumeelezwa kuhusu political parties, jinsi watafanya shuguli zao kwa wakati huu hata devolution of power tumeelezwa vile itakuwa. Tumeelezwa kwa mfano all assets owned by local authority before entering this constitution shall become public property. Kwamba mali yote... si unaona hakuna local authority na wana mali mingi sasa inasemekna hiyo mali yao itakuwa .. Councillor ananiangalia, itakuwa ni mali ya umma hiyo. Lakini si ni yetu hata sasa? Kwa hivyo tunaambiwa hapo for avoidance of doubt wasije wakachukua hiyo ni mali ya umma, na kwamba hiyo property haiwezi kuuzwa ama kupatiwa mtu ye yeyote bila ithini ya serikali kuu. Na pia tunaambiwa Executive wote baada ya katiba hii kuidhinishwa kufikia miezi miwili ni lazima, wafuate leadership and integrity code.

Haya tunaelezwa kuhusu Provincial administration, wanaambiwa hii katiba ikianza kazi yao imekwisha lakini hawatafutwa watarudishwa deployment hakutakuwa na provincial administration. Sasa kuna hiyo maneno mingi tumeelezwa habari ya judiciary. Pengine mungetaka kusikia hiyo kwamba Judge ye yeyote ambaye anafanya kazi kwa wakati huu hatafutwa ataendelea kuwa ni Judge lakini watakao kuwa wamefika miaka ishirini wanaweza ku-retire na wale wamefika 65 sasa ni lazima waende nyumbani. Na kwamba hao Judges ni lazima wa-comply na Ethics na Integrity Commission requirements. Na lazima watafuata ile code ya leadership, na kwamba ikiwa kuna Judge ye yeyote ambaye ameshtakiwa kwa Judicial Service Commission na complaints ye yeyote ya mawakili ni lazima achunguzwe mambo yake ijulikane, na mambo kama hayo. Tunaambiwa about death penalty kwamba mtu ye yeyote ambaye pia amehukumiwa kunyongwa constitution ikianza kazi atafungwa maisha bila kunyongwa.

Sasa hayo ndiyo mambo kwa kifupi ya draft constitution. Sasa kama kuna maneno ambayo mko nayo ambayo mnataka tujadiliane tunaweza kujadiliana; ama mkitaka tufanue tufanye hivyo. Na sio kwa masaa mingi nafikiri ni lazima tujitime tuwapatie 45 minutes kufanya hivyo, na yule anataka kuongea ni lazima akuje haraka ili atumie microphone kwa sababu hii maneno itaenda kuwa recorded isisemekane so and so or Madam so and so aliuliza hivi na akasema hivi. Hapa karibu na dirisha kuna mtu aliinua mkono tafadhali kuja anywhere here at the front. Jina?

Stephen Muoki: Stephen Muoki. Kuna swali Madam Commissioner nilikuwa nataka kuuliza, na hiyo nimeona kama ma-councillors wako. Wakati nilikuwa nataka kusoma hii draft kifungo ile ya powers kuwa devolved – imeandikwa financial arrangement Legislation provision of devolution, page 27 M, inasema mambo ya the cost of salaries of councillors and administrators, unfortunately sijasikia councillor akitajwa anywhere. Niliona imeandikwa salaries za councillors and

administrators na unfortunately sikuona pahali councillors wako, what does that mean?

Com. Abida Ali Aroni: I think it was a topographical era (inaudible)

Stephen Muoki: Na swali ingine, the Bill of Rights section 37 (4) ile inaongea juu ya child mother and father, whether married or not have the obligation of taking care of the child; does it not have a problem when it comes to victimisation that somebody can victimize the other saying that I fathered that child.

Com. Abida Ali Aroni: That is our recommendation as a Commission, can you make your comments or proposal although there are scientific methods of proving who a father is.

Stephen Muoki: So I was of the opinion that the Act or the draft put in place the methods of proving that I am the father of that child so that I am not victimised. That is one. I have got another one in that Bill of rights section 59, about housing section 2 where somebody is not supposed to evict somebody from the house. Now I am suggesting that they should be put in place where the house is, because somebody can decide to go and build on my land without my knowledge and then I don't have money to take him to court; so that he can be evicted from that land and we are not told that somebody should not be removed from the house without the court order.

Com. Abida Ali Aroni: What are you suggesting?

Stephen Muoki: I am suggesting that the draft should find a simpler way, not the court because may be somebody has invaded my land and he has built a house there and I am not able to take him to court.

Com. Abida Ali Aroni: Now, let us take a practical situation if the only place where you can get redress is court, then where can you take the other person for investigation? So for somebody to come to your land and build a home if you read the clause no person may be evicted from their home. Do you know what a home is? How do I come to your land to build a home? You see? That is a very serious matter because if I just came and build a kiosk that is a different thing, but I come to your land to your shamba and build a home. Either I am a squatter for good reason or I am protected by law because there is a law that says if – and it is not against the constitution – if I put up on your land for 12 years without any interruption, I can go to court to be declared an owner. You see? So it is not an easy matter the constitution cannot tell the thief, the court must investigate to know the circumstances. How does somebody establish a home on your land to give you a right to evict that person.

Stephen Muoki: You know why I am saying that is because in African set up there are people who have got land in different places and may be I have a piece of land in Busia where I normally go once in a while and then I can set a family within a month, a home within a month and stay there with my children. So the next month time I go there I find a family there in my

land.

Com. Abida Ali Aroni: You cannot set up a home within a month, I think it depends but we will take your comments because it depends on what a home is. Maybe a house. You can establish a house even within a day but we will take your comments and see how best to sort your concern.

Juliana Muli: Mimi naitwa Juliana Teresia Muli kutoka Kitui division. Mimi niko na maswali lakini si kama maswali ni kama maoni yangu. Vile President amesemekana aende mara mbili kwa bunge awe hawezi kusimama mara ingine. Maoni yangu hiyo sio sawa. Mtu anatakikana achaguliwe na wananchi, ndiyo akiwa anawafanya vizuri hata akienda trip kumi, wenyewe ndiyo wanawenza kuamua kama ni mzuri au ni mbaya.

Hii inasemekana President akichaguliwa awe ni mtu wa university. Tuna wengi wa university lakini reasoning capacity yao sio mzuri inaweza kuwa mbaya. Mtu awe ni mtu wa form 4 anaweza kuongea Kiswahili na Kiingereza awe anaweza kuelewa na wananchi na anaweza kuongea, hiyo sikuona kama ni point ya kufanya mtu asisimame.

Na ingine ni hii kama hii mnasema Assistant chiefs, sub-chiefs, swali ni hii ii village council watakuwa wakilipwa au watakuwa wakifanya kazi ya bure?

Na sasa upande mwingine lakini si kuona pahali waakina mama tunaambiwa tuunganishe wanawake tufanye kama social workers, na hakuna mshahara nayo hiyo ni swali ingine sisi tunaumia hapo, tunaunganisha akina mama, mkiwa mnataka njia itengenezwe sisi ndiyo tunatengeneza na hakuna mshahara. Sijaona mwanaume anatengeneza ni sisi wenyewe. Hiyo ni ingine inatakikana iangaliwe sana.

Sasa wale wengine wanasema mtu councillor, councillor anaweza kuwa aje mtu amesoma hata hajafika std.7. Hiyo ni mtu anakaa na watu wa chini, na anaweza kwenda tuseme hata wakiongea wanawenza kuelewana hata Kiswahili kidogo. Sasa ikiwa ni mtu wa darasa la nane anaweza kuchaguliwa kama councillor, kwa vile huyo ni mtu anayekaa huko reserve. Asanteni kwa kunisikiza.

Com. Abida Ali Aroni: Asante. Nadhania tumesikia maoni yako ingawa tulipokuwa tunachukua maoni ya watu, ndiyo tuliambiwa kuhusu hii term mbili ya President, sijui kama ulihusika kutoa maoni yako kwa wakati huo lakini hivyo ndivyo tuliambiwa na wananchi. Number mbili kuhusu degree tuliambiwa na wananchi na tukaangalia watu wangapi walitueleza hivyo lakini ikiwa mnataka kubadilisha sasa mtaleleza Bw. Councillor na wenzake sasa wakifika huko katika National Conference wajaribu ku-negotiate, na kwa sababu kutakuwa na watu wengine.

Na kuhusu hii village council, ni lazima watalipwa kwa sababu wakatakuwa wakihudumia wananchi kupitia serikali.

Nafikiria mkimaliza kuzungumza mtajiandikisha pale.

Cllr. Munyoki: Mimi naitwa Cllr. Munyoki kutoka Mango. Mimi nataka kusema ya kwamba hii draft yetu tumetengeneza, it is one of the best na nikisema kwa wananchi naona nataka ipelekwe namna hiyo kwa sababu sijui Bw. Commissioner unasilika vile anasema, naona kwa maoni yangu na kwa wananchi tupeleke hii draft ikiwa namna hiyo sababu tumeisoma ndani tukapewa muda na tukiona iko mbaya tunaweza kupeleka mswaada kuitia mbunge wetu warekebishe ama alete maoni ingine kwa bunge. Kwa hivyo tukiletewa hii draft yetu kwa wale watu tulituma kwa district, waende wapitishe na halafu tunasema tunataka kupiga kura 2003 na hii katiba mpya, sababu ni mzuri na inapendekeza na inamwelekeo kwa mwananchi wote. Sisi hatutaki kupiga kura na ile Katiba ya zamani. Kwa hivyo nasema Katiba yetu, hii draft yetu itengenezwe namna hiyo, na iende through. Thankyou very much.

Com. Abida Ali Aroni: Kabla hatujaendelea ningetaka kumtambua mheshimiwa wa area hii, mheshimiwa Katuku, sijui kama angetaka kuwasalimia watu ama tuendelee. Tuendelee. Asante mheshimiwa. Tafadhali utajiandikisha pale tunataka kuandika record ya contributors. Mama tafadhali tumesema mama mmoja na mzee mmoja. Wakikosa wamama tunaendelea na wazee.

Teresia Wambua: Asante sana kwa kunikaribisha hapa kuongea na wananchi. Mimi naitwa Mrs. Teresia Wambua vice chairlady wa district katika Women's group. Mimi ni nataka ku-support ule mwenzangu Mrs Teresia, kwa maana kuna swali nilisikia akiuliza na hiyo hakujimbiwa, ile sisi wanawake tunaunganisha vikundi na tunafanya kazi nyingi sana na hakuna kitu tunalipwa na tunachoka sana. Kule kwingine akina mama wako na taabu sana, saa ingine saa ile wanawachwa na bwana zao wananyang'anya vitu na brothers wa bwana wao na hakuna watu wanawatetea. Hiyo ni kitu tunataka kuuliza.

Na kile kingine hii Katiba tumeenda through na tunasikia ile iko ndani ni sawa. Asanteni sana.

Com. Abida Ali Aroni: Wacha tupate watu watatu wanne ili ndiyo kama nina kitu ya kusema niseme. Huko nyuma kabisa.

Titus Mwasa: My names are Titus Mwasa from Wamunyu, and I thank God for this hour. I want to say something which has been said by somebody before we talk of anything we have to value education, because we are educating our children and this issue is very good when we talk of the President being a degree holder. I think we need to respect that. Let me come to my questions page 22 second column (interjection: inaudible) 175 section 3 ya cabinet. It is recorded the President shall not appoint a Member of Parliament to the office of a Minister or Deputy Minister. My question is, as I read the Daily Nation the other day, it was said that the President was not entitled to elect or appoint a member of parliament and they are not supposed to exceed 15 Ministers. If they are not exceeding 15, not appointed by the president but from the people, how will the procedure take place? Is it per district one person, province one person or which manner?

Second, we are talking of, I can't remember where it is, these equal rights to men and women about inheritance. Were these people considering women who are married or who are unmarried? Do you want to tell me someone who is married when I come back to where I am demand for inheritance goes back and inherits where she is married? And with those few, thank you.

Peter Mutisya: Mimi nasema asante sana kwa kunipatia hii fursa ili niseme machache kwa hii draft constitution. Naitwa Peter Mutisya Katungu kutoka hapa Makutano. It is just my observations I am going to read through. The constitution of the Republic of Kenya draft seems to be well balance but in reality it should be made practical. For example the president of the party in power uses the government's national resources to do his political campaign. The Kenya Police is sure (inaudible) to change the trend. I feel that the police force should be friendly and assisting wananchi but it has become very corrupt that even some members of the force have resulted in performing robberies, instead of checking. A way must be found on the way to change the whole force for the benefit of all the Kenyans.

The proposal that the President or the Commissioner of the police should have a degree from a recognized university should be revisited since an effective leader can be a holder of such papers. Citing an example, the former British Prime Minister, Major had no university degree and he managed to run one of the most successful democratic countries in the world, that is Great Britain. I think one's job ability should be considered. Even the first USA President, George Washington had no degree. Thank you.

Com. Abida Ali Aroni: Jiandikishe pale tafadhali.

John Ndambuki: Madam Commissioner since this concerns politics in some way I will use my political nick name. My name is Capt. John Ndambuki Muthama. Mine is very brief because a previous speaker has put in one of my points; but I will put the other one. On page 9 of the draft constitution chapter 5 paragraph 59, (1) I think we are together now, my feelings about page 9 chapter 5 paragraph 59 (1) is to request the constitutional conference and the draft as commissioners to consider placing the onus of finding adequate housing for Kenyans on the next government. Thank you.

Com. Abida Ali Aroni: Thank you please register.

Willy Kimeu: Thank you once again Madam Commissioner. My name is Willy Kimeu. I had read this draft constitution very thoroughly before and there are a few things I would like you to clarify.

- One, currently there are 22 commissioners, and 10 of them were appointed in 1997 on the agreement of IPPG and they are due for retirement or rather their contract is ending at the end of this month. Then the other 12 were assumed to have been KANU appointees, 3 of those are also due for contractual renewal. Swali langu ni hili Madam Commissioner, hawa macommissioners kumi ambao wanarepresent interest za entire opposition, fate yao ni nini? Hamkusema kitu. There was

some request waongezwe muda but on what strength? Hiyo ni swali moja.

- Swali lingine Madam Commissioner, hii economy yetu ya Kenya as it is now, can it accommodate a 2 chamber National Assembly or Parliament rather, can it accommodate, can it finance 2 chambers na kuna watu wengine wanasemekana 90 wawe appointed na political parties wawe 300 are these appointed MPs whom we are trying to do away with? Au ni njia gani hiyo watakuwa appointed?
- Umeongea juu ya 1/3 of appointed members hawa tuko na constituencies 210, one third ya hawa ni 70 how shall we establish mahali fulani tuchague mwanamke na infact most of the voters madam, and almost 50% of the voters are ladies or past somewhere else they are more like here in Mwala. Now, even ladies themselves don't like ladies, I am talking from 15 years experience akina mama huwa hawapendi wengine, lakini I am not saying ladies wasichaguliwe, how are we going to identify 70 ladies to be elected to parliament? That is another one.
- Kuna kitu ingine inasema President down to Deputy secretary I think kuna mahali inasemekana mtu wa rank ya, deputy secretary rank asihold any political office kwa political party the secretary apart, this deputy secretary is the senior servant and in the laws kuna mahali wanasemekana all public servants they should not be partisan. They should not be associated to political parties. A deputy secretary is a senior civil servant and below is a senior assistant secretary. Hao watu mnataka kusema wawe tunaweza kuhold political posts because that is what the draft is saying.
- Infact I am happy that would have been part of my suggestion when I was presenting. President amesemekana atakuwa anachaguliwa the second, Tuesday of August. This is well and good. The draft constitution is silent on when he should be sworn in. We had proposed because of transition, President asichaguliwe kama leo tuseme second Tuesday of August is fourth, tumalize miezi miwili ndiyo aweze ku-resume office either in October to take charge of office.
- Kuna kitu kingine ambao tuliongea na Commissioners on our past experience wakati wa General Election. The way it looks our General Elections might be held either in December or early January. We had proposed that elections ziwe zikifanywa when there are no rains because it is our government we are trying to save money. Wakati elections zinakuwa held kukiwa na mvua, Madam Commissioner, it is another hell on earth and it is very expensive. Now I don't know whether I am getting on to peoples nerves but there is this abolition of provincial administration. That one I might not be a keen lover of provincial administration, but I think what was wrong with our administration might have been poor supervision right from the top such that these people were not given proper guidelines. We may have to need these people. That is my opinion. I am not saying they are very good but the system is not a bad one. Thankyou Madam.

Jonathan Nzoka: Thankyou very much for this chance. I have only a few points to mention. My names are Jonathan Nzoka one of the wazee's from Makutano market. Nataka kuongea kwa Kiswahili kwa sababu yote yanafaa. Kwanza wakati

nilienda hii draft through, kuna kitu ambao sijakipata kwa uzuri. Sana sana kila mtu nafikiria ako na watoto nyumbani ambao hawana mahali tunakaa tu. Na sana sana katika hii katiba, kwa sababu hakuna kazi ningeuliza Commission ama Katiba makers wa consider watoto sana. Kwa sababu hata tukisema watapatiwa kazi si wote wanasitahili kupata kazi na kwa mfano kama wako katika orodha ya vile wanaweza saidiya ingefaa mzuri kwa sababu kama tuna rural industries tuseme ya aina fulani au fulani; na watu wapatiwe any soft loans ingeweza saidia sana, kwa sababu watoto wetu wana tanga tanga hapa na pale. Wengine wamemaliza masomo hawana njia hawana nini na ndiyo inawafanya hata waibe kwa sababu ukikosa kitu lazima ufanye kingine. Kwa hivyo ningeuliza Commission hiyo iweke katika orodha juu wa watoto iwe namna gani.

Ille ingine ningeuliza, nilisikia kwamba hakuna county council, na hawa watu ndiyo wanamiliki masoko, sasa hii itakuwa ya nani? Who will be the revenue collectors? Hiyo ndiyo pahali nilikuwa nauliza.

Hiyo ingine nilikuwa nasema iwe ya rural industries, sio ati ni hao watoto peke yao hata kuna watu katika nchi ambao kazi ni haba au vile vile kama wengine walivyosema ya kusimamia hiyo project ya (inaudible) kama vile vile serikali ingefanya chochote itoe mchango; tuseme special investments kwa hao watu ambao wako area na ile ile... ingekuwa bora.

Ille ya mwisho ni habari ya maji. Kila mahali ukienda hakuna maji. Kwa mfano leo ukitoka hapa uende kule unakuta watu wanahangaika hapa na pale, na kama ni serikali iangalie kuna zile dams zilinjengwa na wakoloni miaka ya 1920's; na sasa ingine imekwama hata ingine haina maji imepotea na watu wanahangaika. Kwa hivyo hiyo ingewekwa kwenye orodha ingefaa mwananchi. Asante sana.

Stephen Mutunga: Kwa majina naitwa Stephen Mutunga kutoka sehemu ya Mbiuni. Yangu yatakuwa maswali. Swali la kwanza ni kuhusu hii katiba mpya. Baada ya kuangalia nimeona imeleta elections nyingi; na kwa sasa tunaambiwa serikali yetu haina pesa, ninashidwa kama itaweza kugharamia uchaguzi huo wa aina mbali mbali.

Swali la pili ni juu ya Teachers Service Commission, sasa Katiba mpya inasema itawekwa constitutional. Ningependa nielezwe zaidi, sasa itakuwa tofauti namna gani na zamani. Na chini ya hiyo ningependa nielezwe ni nani ata-decide mishahara ya waalimu ile zamani ilikuwa civil servants peke yao na waalimu peke yao. Sasa itakuwa ni chini ya ile Commission kuangalia mishahara ya President na wengine ama namna gani.

Halafu swali ya tatu ni juu ya macommissioners wa CKRC, kuna hili jambo la Majudge kutotaka upande wao uangaliwe na katiba mpya. Ningependa Commissioner utueleze kama wakati ulifika wa jambo hilo, nyinyi wote mlikubaliana mkiwa ishirini na tisa, ama wengine wenu hawakukubaliana na wengine juu ya jambo hilo? Kama Judicial and legal system ya Kenya inapaswa kuwa reviewed na sehemu zile zingine.

Swali la mwisho ni juu ya association. Hapa kwetu ukambani kuna clan associations, tunaona wakati mwingine kama ni chair

person kama wamepanga pesa zitolewe, unaona kama washiriki fulani kwa hiyo clan ya (inaudible) wanatumiwa watu wanaenda wanachukua vitu kwa lazima. Sasa hiyo imeangaliwa katika hii Katiba mpya ama ndiyo namna gani? Asanteni sana.

Evanson Mwaluko: Kwa majina naitwa Evanson Mwaluko kutoka Masii. Mimi singetaka kuongea sana maana nimesoma hii draft tangu last week. Kitu ya kwanza mimi ningesema kwa maoni yangu niko na imani kwa Commission hii ya Ghai; na wananchi hata mimi, tunataka tuende kwa uchaguzi na katiba mpya lakini sio ile katiba ya zamani. Kwa sababu moja, hii inapatia mwananchi uwezo. Inginge katiba mpya ile ya zamani tunaye, ni silent kwa mambo mingi na inatumiwa na mtu kama chombo chake akitaka kuitisha elections kesho anaitisha elections kesho without consulting. Kwa hivyo mimi ningesema nataka tuende kwa uchaguzi na ile katiba mpya. Asante sana.

Com. Abida Ali Aroni: Asante. Sijui kama kuna mtu mwengine? Yes please.

Joseph Muthusi: Asante, mimi naitwa Joseph Muthusi, mimi ni mwalimu. If you look at chapter 5 of the draft constitution, there is something on social security and I was wondering whether the constitution has made a financial provision for the social security expenses granted in that proposal. I was wondering whether it has been found to be economically feasible in our country to support people who are unable to support themselves financially.

On chapter 6 on representation of people we have been told that one third of the candidates for direct election shall be women. My question is what if women candidates are not forth coming? How shall we get them? Because these are direct elections not nominations. In the case of nominations as I have seen there are a good number of women being nominated at least the provision has been made.

Chapter 7, on emoluments of MPs, we have a statement that goes this way, the MP shall not hold any office of profit and goes on like that. My question is what of private practice which is advocates and doctors, can MPs engage in such practice?

Chapter 9 on prerogative of mercy. There is a provision that the President shall only invoke this authority upon advice by another authority. I was wondering whether we shouldn't just live that to the president himself because I don't see any harm in that so far I do not think the prerogative of mercy has been misused by any president in record, so far.

Chapter 12, removal of the office of the Auditor General. Doesn't it look to me like it is too easy to remove the Auditor General by the President because I do not see any restriction.

Chapter 15 on the Defence Forces, when I read the first draft that you provided in that public media, there was a suggestion that our defence force should be given more work but when I read your draft here I do not see a lot of work for the defence forces I was wondering whether we can give them some more work. Most of the time they are largely idle.

Fifth schedule, there is a part known as the fifth schedule in this draft constitution and I wish you could clarify; are we really illegalizing private business for public servants as given on page 45 of the draft constitution?

Then Madam Commissioner if you will oblige me I would like to request you please to explain to us some more about the mixed member parliamentary system it is not very easy to understand though some people said they have understood I am very sure 90% have not understood, me included. Thankyou very much.

Victoria Mutheu: My names are Victoria Mutheu mine is a recommendation. I am of the idea that the present constitution expresses the views of the people, it is well balanced and for example there is a proper decentralization and delegation of powers. It has reflected well on all the people of different categories and so it is my view that it goes through the way it is and just incase of any need of amendments it can be done later in time. Thankyou.

Com. Abida Ali Aroni: Are there more people? Nafikiri tumemaliza maswali. You have something else?

Ngala Musau: My names are Ngala Musau and I have got a few items here for example elections of members of parliament it is said that if a vacancy arise in parliament a by-election should be held. Today it is also like that it does not touch on councils. For example today if a councillor dies we stay for even one year without by-election unless and untill a member of parliament dies. So that one should also include the councils.

The other one is that one of recalling members of parliament. I think 30% ni kidogo sana because if you come to Mwala you realize that the person who was beaten by Katuku had about 12,000 votes which is more than 30% of the registered vote it means such a person can use money and buy people to sign and recall the current MP.

Com. Abida Ali Aroni: What is your opinion?

Ngala Musau: I think it should be more than 51% of the registered voters. The other one is that of dissolving the parliament. There is that one of no confidence the third column on no confidence motion, it is said that if the National Assembly fails the appointment of a Prime Minister within 21 days from the date the vacancy arises the president shall dissolve the National Assembly; but again you find that when we come to the appointment of the Prime Minister the President is also given 30 days after proposing a candidate to dissolve parliament I think that one can be misused, it is better we have 21 days or the 30 days.

Then the last one concerns the current stalemate we hear of, and Madam Commissioner I request you to assure us if Moi dissolves parliament the next week, what will we do?

Com. Abida Ali Aroni: Asanteni kwa maswali nitajibu yale nitaweza, nisioweza kujibu itakuwa sasa bahati mbaya. I will try my best. I think Juliana Muli alikuwa anapendekeza sidhani aliuza tu clarification moja ya village council nikamwambia kwa sababu itakuwa ni utawala wakalipwa. Halafu Cllr. Musyoki nafikiri pia alikuwa anapendekeza kuhusu elections nadhania hivyo ndivyo Tume ingependa; lakini hatuna uwezo hiyo sio kwa kazi yetu kama Tume. Na Mrs. Teresia Wambua alitaka kujua alisema anaona masilahi ya wamama hajashugulikiwa lakini ukisoma article 35 for me I think it is very clear. Article 35 inatuambia kwamba ukiangalia sub-section 5 A and B jinsi ambavyo serikali itashughulikia akina mama na imesema, it will provide reasonable facilities and opportunities to enhance the welfare of women to enable them to realise their full potential and advancement. Nafikiri nikisema reasonable facilities and opportunities you can interprete it to suit what it wants. Kwa sababu sio kila kitu kinaweza sema akina mama wakiorganize groups kuna kitu kinaenda kwa katiba na ile haiendi kwa katiba. Nafikiri pengine hamkuwa mmepeata nafasi ya kusoma but I think hiyo ime... na hata ukiangalia nafikiria kuna kifungu ambayo inazungumza kuhusu family hiyo pia ulikuwa unasema kuhusu family property na marriage nafikiria inasema kwamba katika ndoa both men and women have equal rights. Kwa hivyo ukija kunyang'anywa mali yako utakimbia kortini na pia hapa tumeambiwa katika kifungu 35 men and women have equal rights to inherit. Kwa hivyo nadhania hii mambo iko kwa katiba you just need to be a bit careful in your reading na mambo yote yako hapo.

Halafu kulikuwa na Richard Mwasa, nafikiri nikianza ulikuwa na problem na inheritance women and men having equal rights to inherit, nafikiria hivyo ndivyo tulisikia Wakenya wengi wakituambia ingawa kuna wale walifkiria kama wewe. Now the best you can do is to talk to your representative so that you can try and ammend the draft. Waone kwamba kutakuwa na delegates 629 ambao watakubaliana na wazo lako. Kwa sababu wazo la Wakenya wengi ni kwamba wamama na watoto wa kike hawakufaa kubaguliwa katika urithi wa mali. Sasa sisi tuliandika tulivyo ambiwa na Wakenya. Inaweza kuwa haikukupendeza lakini Waswahili wanasema wengi wape tukafanya hivyo.

Na unasema ulisoma gazette ya Nation ukaelewa kwamba President hatawachagua Ministers kutoka kwa MPs, ndiyo ulisema hivyo? Na hivyo ndivyo hii Katiba inasema, they will be appointed from outside parliament. Ikiwa haikukupendeza sasa pia hapo unaweza kutueleza na ukituma mjumbe wako kwa National Conference utamueleza hivyo kwa sababu umesikia watu wengi hawakufurahia na hayo lakini kama nilivyosema hii ni pendekezo sio sheria, ni pendekezo. Ikiwa unataka MPs watoke parliament mtapendekeza katika National Conference na kwa sasa tutachukua mapendekezo yako tutapeleka huko mbele.

Na nilisahau kuandika jina ya mtu aliyezungumza baada ya Mwasa akatueleza kwamba angetaka hii katiba ambayo ni mzuri sana iwe practical. Na akasema kwamba kwa wakati huu party in power inatumia resources, police are corrupt, president does not need a degree. Sasa hayo ni maoni yako na nafikiria Katiba inatupatia mwelekeo ambao utaweza kuondoa kwa mfano corruption katika Police na inatupatia pia mwelekeo ili chama chochote kiweze kutumia rasilimali ya nchi kwa njia iliyo mbaya. Kuhusu degree nafikiri Wakenya wengi walituambia hivyo but there is still room to give different views kwa hivyo tunatarajia National Conference itaweza kuona kama ni jambo mzuri ama ni mbaya.

John Ndambuki onus of providing house on the government nafikiri sasa tutapendekeza hilo lakini mwakilishi wenu pengine mkizidi kujadiliana mnawenza kuleta jambo hilo katika National Conference.

Na Bw. Willy Kimeu akauliza hawa macommissioner 22 wa commission, although hukunieleza whether ni Electoral Commission I am assuming. Kwamba kuna wale kumi wakati wao utaisha. Unajua Bw. Kimeu kwa wakati huu Kenya iko na sheria. We are not living in a vacuum. Tuko na sheria ambayo itatekelezwa kabla hii katiba haijakuwa into force unless parliament, hata tuko na bahati tuko na mheshimiwa hapa pengine wao watafikiria vile watafanya lakini hiyo sio jukumu ya Review Commission. Kwa hivyo lazima kuwe kuna sheria ya kusema vile mambo itafanyika. Hatuko kwa vacuum unless our MP here and his colleagues change. Kwa hivyo tutaendelea kuzungumza na yeze tuendelee kuona vile watafanya. Watatusaidia kwa hayo.

Na pia ukauliza kama economy ya nchi yetu inaweza kusimamisha hizo nyumba mbili. Nadhania sasa hayo ni maneno tumerudishia nyinyi kwa sababu nyinyi ndiyo mltuambia. Mltuambia mnataka bi-cameral na sisi tulimletea vile mltuambia, je mkiona haiwezi katika National Conference watu wakijadiliana matatueleza halafu hao wakiliishi ambao watakuwa ni watu zaidi ya mia sita wataona na kutatua hilo jambo. Hii ni swali muhimu ambalo umeuliza na pengine litazingatiwa katika National Conference.

Na ukauliza hao watu watakaochaguliwa na political parties, hiyo list yao watakuwa nominated au la. Nafikiria unaweza kusema kama ni nomination through the parties. Nominations na wameelezwa masharti watakayofuata kwamba wanatakiwa wapatie priority na wajaribu kufanya, waonyeshe National character na kuziba loophole ambayo iko katika elected MPs. Na ukauliza je hii 1/3 appointment vipi 70 watakuwa ni wanawake? Ukiangalia section 109 inasema kwamba ni juu ya parliament kufikia miaka mitatu ijayo wakati ambapo hii katiba mpya itakuwa into force kuweka sheria itakayo hakikisha kama tuna 1/3 representation of women. Hiyo itakuwa ni jukumu la parliament kuhakikisha kwamba kuna wamama 1/3 na pia ukasema kwamba je wamama wanachukiana ni kweli mzee lakini ukiangalia historical and cultural position ya nchi yetu si rahisi kwa wamama kupigania kura kama wanaume. Wewe unaweza kuenda pale kwa jukwaa ukasimama na ukapigana vita mama bibi yako nyumbani hawezi hayo, si ni ukweli? Kuna mambo mengi, halafu culture wamama tuliambiwa miaka mingi kwamba kazi yetu ni jikoni. Sasa kubadilisha hiyo mawazo mzee itachukua miaka mingi. Ni kitu kimefanyika ulimwengu mzima hata tukiangalia saa hii ukiangalia America wamama ambao wako kwa bunge huko sio wengi, ndio kila pahali, the whole world ndiyo sasa kunafanywa kitu kinaitwa affirmative action. Na ukiangalia hata wamama hawasemi wanataka nusu kwa nusu, hapana. Wanasema hakuna nyumba inajengwa na mtu mmoja hata wewe ukikuwa peke yako kwa nyumba huwezi kulea watoto, si ni lazima uwe na mama mnashirikiana? Sasa tunasema nchi haiwezi kuwa na sauti na mafikira ya baba peke yake na kuwacha wamama nje. Kwa sababu hataangalia huko kwenu kwa kijiji. Mzee saa hii mkiwa na meeting muangalie development wazee wanawenza kusema sasa kitu ya maana pengine tupatiwe stima kwa sababu usiku tukitoka kwa club kuna giza. Mama akiwa kwa huo mkutano atafikiria maji. Umeelewa mzee? Huwezi kujenga nchi na wanaume bila wanawake upende usipende, ndiyo maana imesemekana tuwapatie wamama nafasi waingie parliament, washikamane na wazee, waweke

fikira za watu tofauti. Si Mungu aliumba Adam akaona hatoshi akaumba hawa, sindiyo? Basi na pia wamama wanasesma hata Bunge ni lazima wakuwe huko waweze kujenga nchi. (interjection)

Speaker: I was not opposing the ladies what I was saying hawa akina mama 1/3 watachaguliwa, wao wenyewe watachaguliwa?

Com. Abida Ali Aroni: Haiwezekani mzee. Kwa miaka thelathini na tisa, arobaini saa hii tuko na wamama wangapi parliament? Wangapi wamekuwa elected? It is not possible. 7 wengine ni nominated, it is not possible from history, sasa kulingana na maoni tuliyopata tunasema wamama wafanyiwe affirmative action siku ile watazidi siku hiyo.

Na pia ukauliza kuhusu civil servants, na ukasema kwa nini tunasema deputy, secretary kuenda juu, je wale wengine si ni civil servants? Ukiangalia article 48 inawapatia watu right of association, sindiyo? Inasema unaweza ku-associate na mtu yeoyote. Ukiangalia kifungu ya political parties, inawapatia Wakenya uhuru wa kujiunga na political parties. Sasa tukiambia civil servants wote, msiingie kwa political parties, situtakuwa tumeenda kinyume na sheria? Ndiyo tulisema mbeleni kwamba utapatiwa haki ya kimsingi lakini wakati mwingine kwa sababu ya maslahi ya nchi unaweza kunyang'anya freedom hiyo. Lakini huwezi kunyang'anya ... hata messenger kwa ofisi unamwambia don't join a political party nani atapiga kura sasa, mzee? Siunaona iko shida? Sasa wale deputy secretary and above ni kwa sababu ya kazi yao ile wanafanya. Wakiwa wanahold positions wakati mwingine, si wewe unasema ama mwenzako amesema serikali ya wakati huu inatumia mali ya umma ndiyo sasa tunasema watu ambao wako na cheo ya juu wasipewe nafasi ya kutumia mali ya umma, ama kufanya decisions ambaye itapendelea kikundi kimoja ama kingine. Lakini mwananchi wa kawaide aweze kuwa na freedom of association, political freedom as well.

Lakini ukiona Permanent Secretary ako juu na una ... wengine pengine unaweza kupendekeza. Lakini hatuwezi kusema all civil servants, otherwise party itakuwa haina members. Ama unataka isiwe na members? They are holding office kwa sababu watakuwa na interest na mimi nikiwa Chairman ya party na niko na cheo kubwa kwa serikali, si unaona saa ingine unaweza kupendelea upande wangu. Hiyo ndiyo tunataka kuondoa kwa wakati huu. But not all civil servants have the ability prefer certain things to their political party. Si niukweli ama sio hivyo? Sasa tumeelewana?

Na umesema kwamba swearing of the president iko silent; na elections should not be during the rainy season. Sasa unajua mambo ingine ni ngumu hii ya elections. Kwa sababu, sijui kama November iko mvua? Sasa pengine kwa National Conference utatuma mwakilishi wenu apendekeze siku ile mzuri. Kwa sababu hii tumeweka date hapa lakini nilisema ni raw draft tunaweza kubadilisha tukielezwa siku hiyo ni mbaya tuweke siku ingine. Kwa hivyo hii sio final na pia hiyo swearing tutapendekeza tuone kama iko loophole halafu tuone kama tunaweza kurekebisha.

Jonathan amesema kwa vile hakuna county council, ni nani atakuwa anachukua mapato sasa ni nani ataangalia market. Ukiangalia ile schedule huko nyuma inayotoa kazi za hizi vyombo vitakavyokuwa vya utawala tunaambiwa kwamba district

council itashughulikia market and trade centres. Kwa hivyo hiyo kazi itafanya na district council na ataongea kuhusu maji. Nafikiri katiba imependekeza kwamba wananchi wote wapate maji safi na maji ya kutosha. Kwa hivyo hilo ni jambo limezingatiwa.

Kulikuwa na Mr. Stephen Mutunga anasema kwamba there are too many elections sijui kama alikuwa anapendekeza gani angetaka iondolewe katika zile tumependekeza na aauliza sasa TSC sasa imewekwa katika Katiba sasa itakuwa na tofauti gani? Hapo mbeleni TSC haikuwa kwenye Katiba na tumesema wacha tu-safeguard the existence of TSC na ipewe majukumu yake iwe katika Katiba kwa hivyo imewekwa na aauliza kuhusu salaries. Nafikiri waalimu wako chini ya civil service na mishahara yao inashughulikiwa katika civil service kama wengine na ile Remuneration Commission imepewa jukumu lake kulingana na vile tumependekeza. Kwa hivyo sidhani waalimu wako hapo.

Na aauliza swali kuhusu recommendations of the Judges, whether the Commissioner were together. Sijui nitakujibu vipi, lakini decisions of the commission are normally done by consensus or by voting. It doesn't matter whether all Commissioners are together. Consensus means majority. If 20 Commissioners agree on a view whether the other 7 who vote agree or not the view of the majority comes and that is how we make our decisions without going into details. Pengine kuna wale hawakufurahia recommendations, lakini we either vote or by consensus.

Halafu Bw. Evans alipendekeza, kulikuwa na Joseph Muthusi alitaka kujua hii social security kama kuna pesa za kutosha kufanya mapendekezo hayo. Nafikiri constitution inasema it is the duty of the government if that recommendation passes through the National Conference; I think it will also be the duty of the government to look for the funds to take care of that.

Na aauliza hii section ambayo inazungumza kuhusu MPs na emoluments ama mishahara yao na wao kukatazwa kufanya kazi. If you read carefully, section 121 it says any activity that is likely to jeopardize their work I think if you are a doctor surely and you are an MP by treating people you are not jeopardizing your work. If you look at sub-section 2 a member of parliament shall not hold any office of profit or engage in any activity likely to compromise members office. I think you will just need to read and understand that section.

The others were comments on prerogative of mercy, I think we will take your comments as they are. Auditor General you feel that kumuondoa ni rahisi but I wish you had come up with a proposal and you can give it to your representative and also your proposal. We got a few people who gave us proposals that the defense should be involved in other work. I think those were proposals our draft did not bear that and I can assure you that after wide consultations and research elsewhere we came up with that proposal; but if you think otherwise I think you can send your representatives with proposals that can sell to amend the draft. Nafikiria hayo ndiyo majibu ambayo ningependa kuwajibu kwa wakati huu.

Mutuku Mueke: Kwa jina naitwa Mutuku Mueke na nina swali sijui nielekeze kwako ama kwa MP ambapo Rais anasititisha

kwamba tutaenda uchaguzi na Katiba iliyoko. Je kama tukienda uchaguzi na Katiba iliyoko, na baadaye hii katiba ambaye ni draft, iwe approved na parliament which will be sitting at that time tutafanya uchaguzi tena ama tutafanya aje? Hilo ni swali ambalo niko nalo na mtuma MP wetu anakuuliza utujibu kama lawyer.

Com. Abida Ali Aroni: Bw. Mutuku nadhania katika terms of reference ya Commission hatuhusikani na mambo ya uchaguzi, kwa hivyo sidhani ningeweza kujibu swali hilo nafikiri, hilo ni swali la either Electoral Commission or Parliament, tafadhali. Sisi tumefanya kazi yetu tuliopewa kufanya and we are still working. Hatuna nguvu ya kuita election, or otherwise we are like the rest of you, tafadhali. Wacha tuombe Mungu tumalize ndiyo mambo mengi yasifanyike. I don't know whether the Honourable MP would like to address us.

Hon. Katuku: Kwanza ningependa kushukuru Mwenyezi Mungu kwa kutupee nafasi hii tukiwa hapa leo. Pili nishukuru Commissioner wetu na wafanyi wetu wa Commission, kwa kutenga siku ya leo kukutana na wananchi wa Mwala kuhusu maneno ya Katiba, hiyo tunasema ni shukrani kwa vile mmekuwa na patience mpaka wa sasa. Kama vile mnajua hii katiba ni kitu muhimu, leo nilikwa niwe Mombasa lakini nikatisha safari yangu yakuenda Mombasa ili niwe na nyinyi kusudi nisikie vile mnaiona kwa vile tutaenda kwa hiyo Constitutional Conference; na kama mwakilishi wa eneo hili nitakuwa na nafasi mzuri nikiwa ninasikia mnasema namna gani. Kuna mambo mengi yametanjwa na watu tofauti tofauti, na ninataka kuamini ya kwamba watu wengi hawajawahi kupata hii nakala ya hii draft. Wengine wameipata leo na wale wanapata magazeti ni wachache ilikuwa kwa Daily Nation na ilikuwa hapo ndani. Lakini machache huko mashinani, grassroot ambao wanapata nafasi ya kusoma magazeti lakini leo wengi wetu wemepata nafasi ya kupata copy.

Ile ningewaomba ni kwamba muende muisome vizuri hata sasa nafikiri ile mmetoa hapa ni ile ya juu juu. Ukienda uisome vizuri na uone jambo muhimu sana unafikiria hii inapaswa kuzungumziwa katika constitutional conference, uko na uhuru wa kuandikia hii Commission, naona kama iko hivyo ama kuniona ama kuona wakilishi wale wengine kwa vile hiyo itakuwa na wakilishi kama mia sita, na wajumbe watakua mia mbili na ishirini. Wale wengine wanatoka sehemu zingine, councils, wengine wanatoka civil societies hivo hivo. You can see any of those people. Ama unaweza kumuona mmoja wa hawa kama mimi, ili wazo lako lile unasikia haijawakilishwa vizuri kwa draft ambayo tuko nayo tukaijadili.

Ni mambo mingi hapa ambayo inaweza kupinduliwa ingine kuongezwa ingine kutolewa lakini tutategemea wale wataenda huko constitutional conference watakuwa prepared on these issues. Kwa hivyo ndivyo na mwambia ikiwa uko na issues tafadhali nione kwa ofisi. Every Monday nakuwanga Masii, saa saba, every Monday nakuwanga Athii at the office there saa nne, ukija hapo tujadiliane hiyo kabla hii date ya constitutional conference utapata nafasi ya kuwa umewakilishwa kwa hiyo.

Hii maneno ya Katiba, is a political process, na ndiyo unaona iko hivi na hivi lakini ningipenda kuwashukuru Commissioners kwa kazi ile mzuri mumefanya. Hii mmewardhika na vile hii draft ya Katiba yenyewe, haya ni maoni vile yalikuja tutaenda ku-convince each other; maybe you have a different opinion than yours na ukiniconvince unakuja karibu moja. Kwa hivyo

nilikuwa nataka kusema mimi na shukuru kazi ile Commission walifanya isipokuwa ni kuwa na mambo mingi, wakati wa kutoa maoni hata I remember at one time when we were here vile watu wanapaswa kuja kutoa maoni wengine wanasema msiende huko and this is a political process lakini tumeenda tumefika pahali tumefika sasa tuko na draft ambayo tunasema tunaweza kujadiliana. Mbeleni haikuwa na draft ndiyo nasema nawashukuru vile mlikuja kutoa maoni yenu Commissioners walifanya kazi yao na ugumu ile ilikuwa mpaka mahali mmeefika.

Kwenda mbele mpaka mwisho that is also a political process. Tumefika mahali lakini kuenda kufika mwisho iwe sheria is also a political process. Utasikia mheshimiwa Katku anasema hivi, utasikia Moi anasema hivi, utasika Ngilu anasema hivi, Wamalwa hivi na viongozi ni lazima waseme. Hata wewe ni lazima useme. Onukhu amesema hapa anataka twende uchaguzi na Katiba mpya, sijui nani amesema anataka tuende uchaguzi na Katiba hii mpya. That is a political statement. It is your wish and it is also my wish. Na pengine kuna mwingine anafikiria mengine na tuna katiba ile iko. Ile tunasema ni kwamba it appears that the majority of Kenyans want to go to the elections with a new constitution.

Saa hii tunaongea, kamati ya Bunge ile inahusika na hii Katiba, sasa wakutana Mombasa wako kwa mkutano saa hizi na wakilishi na Commissioners wengine ndiyo kamati iko hapa, ikijadilia kamati iko hapa. Hiyo ndiyo agenda moja wanajadilia apart from being briefed on the constitution on how to go about it, hiyo ni moja ambayo ya swala ambalo wanaongea. Tutaenda na katiba mpya au mzee. Moi anasema ni mzee wengine wanasema ni mpya, wewe unasema nini? Kwa hivyo hiyo ni maoni yako, na ya Moi ni yake, na yangu ni yangu; na kila mtu ako na uhuru. Lakini kwa Katiba ambaye tuko nayo kama vile Commissioner amesema, hatuko kwa vacuum tuko na sheria, ili sasa tulijaribu Bunge kukata hizo powers za President akatushida na watu wengine wakatushida. Sasa tumeleta mswaada ingine sasa through mheshimiwa Aloo Aringo ya kujaribu kukata hiyo tena asijaribu kuvunja kabla hatujaweka hii.

Na ndiyo nasema hii ni political process, tutajaribu vile tuwezavyo tuone tutamconvince akubali tuende na hii. Isipokuwa kuna maswali mengi hapo, utasikia wakisema lazima tuende na mpya basi na bunge isongezwe. Utasikia wengine wakisema hapana, nataka kuwe mjambe pia mimi. That is why I am saying it is a political process, na ni lazima tuiangalie namna gani... lakini kulingana na vile hawa wametufuatisha ni kwamba is that unless parliament is dissolved before sometimes 15th December, it will be through this process. That is what we want to imagine. But then we don't have the powers, we don't know whether we will get there; but we are trying our best to put pressure and convince that kind of process that we can get there.

So hiyo maneno ya tutaenda mpya, hatutaenda mpya ni political process. We hope, my appeal is that and I would want to appeal to the President those who are opposed to this new constitution to see the wishes of Kenyans. Wengi wetu tunataka Katiba mpya hiyo ndiyo ningetaka kuomba Rais hapa pahali ako afikirie mafikira ya watu wengi. Kwa hivyo kwa hayo machache kwa vile nimesema hii ni political process; maoni yangu umesikia ni kama hayo yako wewe. Kuna mwingine fikira anasema vingine lakini mimi nasema vile unasema Katiba mpya lakini hata tukiongea saa, hii bunge yaweza vunjwa hiyo ako na huo uwezo wa katiba ile mzee. Kwa hivyo tunaomba tu asivunje kabla ya hata hii Constitutional Conference iko at the end

of this month. Tunaweza kosa kufika huko ndiyo nasema muombe sana wengine siasa hapa na pale tuone kama inawezekana. Asante sana. (clapping)

District Coordinator: Asante sana watu wa Makutano, watu wa Mwala, kwa wakati mzuri tumekuwa na nyinyi: na kwa wakati huu kwa maana hatuna na mengi ya kusema ningetaka tufunge mkutano wetu kwa leo, na wacha niseme kwamba ni asante sana kwa uvumilivu wenu, tumekaa sana wengine wetu tumekuja tumechelewa lakini tumeshukuru maoni yenu tumeyasikia na kulingana na vile mheshimiwa anasema kuna wengine watu wale watakuwa wanaenda kwa Constitutional Conference. Pengine mheshimiwa Katuku hutaweza kupata nafasi ya kuenda kwake, lakini kwako ni karibu na Cllr. Musau, na amesema ni mmoja wa wale wamechaguliwa na pia tunabahati tumpata pia mwingine Victoria Mutheu, ni mwingine ambaye amechaguliwa pia kutoka kwa area hii. Mutheu tafadhali simama watu wakaweze kukuona. Mutheu is a lawyer by profession. Sasa hao ndiyo watu wengine tunaweza kuona na tukawapatia maoni yetu kulingana na draft constitution, yale mambo tungependa yabadilishwe ama mambo mengine tungependa yaongezwe kwa katiba mpya. Kwa hivyo hebu nikasema tukajipigie makobi kwa kukaa mpaka wakati huu. Nani atatufungia mkutano kwa maombi sasa? Asante, mama, karibu.

Maombi:

Tuombe: Kwa jina la Baba la Mwana la Roho Mtakatifu. Mungu nimekurudishia asante kwa kutuwezesha kuwa hapa tangu tuanze mkutano huu tukiwa na Commissioner wetu Madam, tunamrudishia asante kwa kuja kutuonyesha vile tunaendelea na tunaomba tuendelee hivyo na tuwe pamoja nawe. Mungu tunakuomba hiyo yote kwa njia ya Bwana Yesu Kristo Mkombozi wetu. Kwa jina la Baba la Mwana na Roho Mtakatifu, tumeshukuru Mungu milele na milele, Amina.

District Coordinator: Kabla hatujaenda tafadhali kuna watu nataka kuona, Cllr. Victoria Mutheu, Members of the Committee don't go, civic education providers wenye wako don't go tafadhali.

Meeting ended at 2.30 p.m.

&&&&&&&&&&&&&&&&&&&&&&